Haliuzwi
AGOSTI 3, 2026
/islamicftz
Safar 18 1448

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 595

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Joto lafikia nyuzi 50 UAE, nchi 10 Mashariki ya Kati zaathirika

# Mahaad za Kiislamu zaazimia kuja na mtaala mmoja

"Mtaala mmoja utasaidia kuandaa wahitimu wenye elimu sahihi ya dini, malezi bora na maadili mema yatakayochangia amani na maendeleo ya jamii." - *Aref Nahdi, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation*



## Samia: Amani ndiyo injini ya matarajio ya uchumi wa $1 Trilioni

"Mimi kama kiongozi wa Serikali ni mshumaa. Kazi yangu ni kuwaka, kutoa mwanga huku nateketea, lakini umati unafurahi. Hiyo ndiyo kazi yangu. Kwa hiyo nitaendelea kuwa mshumaa mimi na mwenzangu hapa Rais Dk Mwinyi, tutaendelea kuwa mshumaa." - *Samia Suluhu Hassan*



**MAKALA**

**Adui yetu mmoja, misimamo tofauti: Wito wa tafakuri mpya kwa Waislamu**

**MAKALA**

**Hafla za qasida aina hii zisina sibishwe na Uislamu**

## Mwinyi asifu maono ya Samia, awataka viongozi kubadilika

- Aweka msukumo mpya wa Serikali ya kidijitali, ahimiza viongozi kwenda na wakati, si masuala binafsi



## Matumaini amani Gaza Hamas ikilegeza msimamo

NA HASSAN NINGA, MOROGORO



# Mahaad za Kiislamu zaazimia kuja na mtaala mmoja

**■ Amiri wa Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA), Sheikh Ally Zubeir, amezitaka taasisi zote za Kiislamu kuwa tayari kuutekeleza mtaala huo mara utakapokamilika, akisema hatua hiyo itasaidia kuinua viwango vya elimu na kuleta manufaa kwa jamii.**

Katika hatua inayotarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika mfumo wa elimu ya Kiislamu nchini, viongozi wa Mahaad za Kiislamu kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania wamekutana mjini Morogoro kujadili uanzishwaji wa mtaala mmoja utakaotumika katika vyuo hivyo, kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu, nidhamu na mfumo wa mitihani unaofanana.

Kikao hicho cha kwanza kinafanyika katika Shule ya Sekondari ya Forest Hill, kikiwa na lengo la kuweka msingi wa mfumo mmoja wa ufundishaji utakaosaidia kuandaa wahitimu wenye elimu sahihi ya dini ya Kiislamu, maadili mema na uwezo wa kulitumikia taifa na Umma kwa ujumla.

Mkutano huo umeandaliwa na Umoja wa Mahaad za Kisunna chini ya Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA), kwa uratibu wa taasisi ya The Islamic Foundation na kwa ufadhili wa Jumuiya ya Mkusanyiko wa Vijana wa Kiislamu Duniani (WAMY).

Mbali na kujadili mtaala huo, washiriki pia wanapatiwa mafunzo ya kuongeza umahiri wa walimu katika ufundishaji na kuimarisha uongozi wa taasisi za elimu ya Kiislamu.

Akifungua kikao hicho, Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amesema kuwa mtaala huo utakuwa chachu ya kuandaa wanafunzi wenye elimu sahihi, malezi bora na maadili mema yatakayochangia kudumisha amani, mshikamano na maendeleo ya jamii.

"Mimi nakumbuka wakati wetu sisi huwezi kutoka maahad moja kwenda nyingine kwa sababu mitaala inatofautiana. Hivyo umoja wa hizi maahad unasaidia sana katika maadili, kwa mfano kuzungumzia amani. Inakuwa ni rahisi wakihitimu kuwa na uelekeo mmoja wanapoenda kufanya dawah," alisema.

Nahdi, ambaye taasisi yake inamiliki maahad katika mikoa mbalimbali nchini, alisema lengo ni kuona mtaala huo ukitumika si Tanzania pekee, bali pia katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki.

Aidha, Mwenyekiti Nahdi pia alisdma lengo la Umoja huo wa Mahad za Kisunna ni kushawishi mtaala huo utakaopatikana utambulike Serikalini na uweze kutumike katika shule mbalimbali.

Kwa upande wake, Amiri wa Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA), Sheikh Ally Zubeir, amezitaka taasisi zote za Kiislamu kuwa tayari kuutekeleza mtaala huo mara utakapokamilika, akisema hatua hiyo itasaidia kuinua viwango vya elimu na kuleta manufaa kwa jamii.

Naye Mwenyekiti wa Mpito wa Mahaad za Kiislamu nchini, Sheikh Ally Nassoro, amesema kikao hicho pia kimetoa fursa kwa viongozi wa Mahaad kupata mafunzo ya uongozi bora yatakayowajengea uwezo wa kusimamia taasisi zao kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Ukhty Shamsa kutoka Tanga, alisema kuwa mtaala huo utasaidia kuandaa kizazi chenye elimu sahihi ya dini, hususan wanawake watakaokuwa na mchango mkubwa katika kujenga familia zenye maadili na jamii yenye misingi imara ya Kiislamu.

Washiriki wa mkutano huo wameeleza matumaini kuwa makubaliano yatakayofikiwa yatafungua ukurasa mpya wa kuimarisha elimu ya Kiislamu nchini kupitia mtaala unaozingatia ubora, umoja na maadili.

صَفَر



# MATUKIO KATIKA PICHA


Na abdulrahman Omar

0655 763 580

## Mkutano Umoja wa Mahaad za Kisunna chini ya Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA)











صفر

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Samia: Mtaji wa kwanza ni amani, si fedha

Serikali na sekta binafsi wamekubaliana kutekeleza hatua 24 zitakazolenga kuharakisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050 na kufanikisha azma ya kujenga uchumi wenye thamani ya dola trilioni 1 ifikapo mwaka 2050.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika mazungumzo ya ngazi ya juu kati ya Serikali na sekta binafsi yaliyoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambapo pande zote zilikubaliana kuwa kufikia malengo makubwa ya maendeleo kunahitaji ushirikiano na uwajibikaji wa pamoja.

Hatua hizo zimegawanywa katika maeneo matatu makuu; ahadi nane za Serikali, ahadi nane za sekta binafsi na maeneo nane ya utekelezaji wa pamoja.

Mpango huo unalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuongeza ajira, kukuza viwanda, kuongeza thamani ya bidhaa, kupanua mauzo ya nje, kuimarisha biashara za ndani na kuongeza ushindani wa Tanzania katika uchumi wa kikanda na dunia.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dk. Fred Msemwa, alisema mafanikio ya Dira ya 2050 hayawezi kupatikana kupitia juhudi za Serikali pekee bali yanahitaji mchango mkubwa wa sekta binafsi.

Alisema ushirikiano wa karibu kati ya Serikali na wafanyabiashara utakuwa muhimu katika kudumisha ukuaji wa uchumi, kuongeza uwekezaji na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji na biashara Afrika.

"Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, uwekezaji na ajira, kuimarisha viwanda na biashara za ndani, kuongeza mauzo ya nje, kuboresha ushindani na kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wananufaika na ukuaji wa uchumi," alisema Dk. Msemwa.

Chini ya makubaliano hayo, Serikali imeahidi kudumisha utulivu wa uchumi, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kuhakikisha sera zinakuwa na uhakika, kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati na kuimarisha taasisi za umma.

Serikali pia imeweka mkazo katika kuendeleza viwanda, kuongeza thamani ya bidhaa za ndani, kuwekeza katika elimu na ujuzi wa wananchi pamoja na kuimarisha mifumo ya mawasiliano na sekta binafsi.

Kwa upande wake, sekta binafsi imeahidi kuongeza uwekezaji, kuunda ajira zenye staha, kuchochea ubunifu, kukuza viwanda, kuongeza mauzo ya nje na kuimarisha biashara zinazomilikiwa na Watanzania.

Sekta binafsi kubeba asilimia 70 ya utekelezaji

Rais Samia alisema sekta binafsi itakuwa mhimili mkubwa katika utekelezaji wa Dira ya 2050, huku ikitarajiwa kubeba takribani asilimia 70 ya majukumu ya mpango huo.

"Sekta binafsi imepewa takribani asilimia 70 ya utekelezaji wa dira hii tunayozungumzia kwa miaka 25 ijayo," alisema Rais Samia.

Alisema Serikali itaendelea kuboresha sheria, sera na taasisi ili kujenga mazingira yatakayovutia uwekezaji na kuruhusu biashara kukua kwa uhakika.

Rais Samia pia alitaka kuimarishwa kwa uhusiano kati ya kampuni kubwa na ndogo, huku akitaka biashara zisizo rasmi kusaidiwa kuingia katika mfumo rasmi wa uchumi.

Aliwataka vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kushiriki zaidi katika shughuli za uzalishaji ili kuhakikisha ukuaji wa uchumi unawanufaisha wananchi wengi.

Alisema Tanzania inapaswa kutumia nafasi yake ya kijiografia, bandari, reli na fursa za Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kufungua masoko mapya ya bidhaa zake.

"Tanzania ina nafasi kubwa ya kuwa kitovu cha uzalishaji na usambazaji Afrika, lakini tunahitaji kuhakikisha bidhaa zetu zinafika kwenye masoko ya nchi jirani," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan akijadiliana jambo na Waziri Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba kwenye hafla ya uzinduzi wa nyenzo za utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, jana. Picha na Ikulu

صفر

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU




# Samia atoa dira, Mwinyi ataka viongozi wawe sauti ya Serikali

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kusisitiza umuhimu wa kuimarisha uwezo wa Serikali katika mawasiliano, uwajibikaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo, hatua ambayo imezaa semina elekezi kwa viongozi wakuu wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza wakati wa kufunga semina hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alimpongeza Rais Samia kwa maono na maelekezo yake ya kuandaliwa kwa mafunzo hayo, akisema yameongeza uelewa wa viongozi kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya mawasiliano na mahitaji ya sasa ya wananchi.

Rais Mwinyi alisema semina hiyo imewajengea viongozi uwezo zaidi katika kuwasiliana na wananchi, kueleza sera na mipango ya Serikali, pamoja na kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Aliwataka Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutumia mbinu za kisasa katika utoaji wa taarifa, ikiwemo matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii, ili kujenga uelewa na imani ya wananchi kwa Serikali.

"Mawasiliano ni nyenzo muhimu ya kujenga uelewa na imani ya wananchi, kuimarisha taswira ya Serikali na kuelekeza mijadala ya umma," alisema Rais Mwinyi.

Alisema viongozi wanapaswa kutanguliza wajibu wa kuisemea Serikali na maslahi ya umma badala ya masuala binafsi, huku wakizingatia kwa makini ujumbe wanaoutoa pamoja na mwenendo wao katika majukwaa mbalimbali ya mawasiliano.

Rais Mwinyi aliwataka viongozi kutumia kikamilifu vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi kueleza sera, mipango na utekelezaji wa Serikali, kutoa elimu kwa umma na kukabiliana na taarifa potofu.

Alisisitiza kuwa kabla ya kuzungumza na wananchi, viongozi wanapaswa kujiandaa ipasavyo ili kuhakikisha wanatoa taarifa sahihi, zenye kujenga na zinazoeleweka kwa jamii.

Aidha, Rais Mwinyi alisema mabadiliko ya teknolojia, matumizi ya mitandao ya kijamii na maendeleo ya akili unde (AI), pamoja na mabadiliko ya siasa za kimataifa, yamebadili namna Serikali inavyopaswa kuwasiliana na wananchi, hususan vijana ambao ndio sehemu kubwa ya watumiaji wa majukwaa ya kidijitali.

Kuhusu Muungano, Rais Mwinyi alisema semina hiyo imeongeza uelewa wa viongozi kuhusu misingi na umuhimu wake, huku akiwataka kuendeleza ujumbe unaojenga umoja wa wananchi na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema viongozi wana wajibu wa kuuenzi Muungano kama msingi wa Taifa imara na kuhakikisha mawasiliano yao yanachangia kujenga mshikamano wa kitaifa.

Semina Elekezi kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanyika kwa siku mbili katika Hoteli ya Golden Tulip Airport, Zanzibar, ikiwa imelenga kuwaongezea viongozi uelewa kuhusu mawasiliano ya kisasa, uwajibikaji na mwelekeo wa maendeleo ya Taifa.

MAHMOUD NYAMGUMA

# Rais Samia asukuma ajenda ya maridhiano

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itaendeleza maridhiano ya kisiasa nchini kuelekea hatua za maboresho ya Katiba kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. Katika kuyatimiza hayo, ameahidi kuendeleza majadiliano na vyama vya siasa ili kujenga mwafaka kuhusu masuala muhimu ya Taifa.

Rais Samia ameyasema hayo Julai 30, 2026 alipokutana na viongozi wa vyama 18 vya siasa nchini katika mkutano uliofanyika Ikulu, Dar es Salaam. Mkutano huo ulijadili maridhiano, mageuzi ya kisiasa, uchumi, huduma za jamii, ajira, uwekezaji na ulinzi wa amani.



Katika hotuba yake, amegusia maridhiano ya Zanzibar, akisema Serikali inaendelea na maandalizi ya hatua zinazofuata za mapitio ya Katiba na kwamba kila hatua itazingatia misingi ya sheria na maslahi mapana ya Taifa.

“Mchakato huu unahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali wa kisiasa na kijamii ili kuhakikisha unafanyika katika mazingira ya amani, utulivu na uwajibikaji,” alisema Rais Samia.

Aidha, alisema Serikali itaendelea kukutana na viongozi wa vyama vya siasa angalau mara tatu kwa mwaka kwa lengo la kuimarisha mazungumzo, kujenga uelewano na kutafuta suluhu za masuala yanayohusu maendeleo ya nchi.

## Kuhusu uchumi

Katika hatua nyingine, Rais Samia amezungumzia hali ya uchumi wa nchi, akisema umeendelea kukua kwa asilimia sita mwaka uliopita, huku ukuaji wa asilimia 6.3 ukitarajiwa mwaka huu. “Serikali imeelekeza nguvu katika kukamilisha miradi mikubwa ya maendeleo iliyoanza kutekelezwa, pamoja na kuendeleza uwekezaji katika miundombinu ya kimkakati,” alisema Rais Samia.

Katika sekta ya uwekezaji, amesema maboresho yaliyofanywa katika Bandari ya Dar es Salaam yameongeza uwezo wa kuhudumia biashara ya ndani na kikanda.

Aidha, amewataka viongozi wa vyama vya siasa kulinda amani, uhuru na maslahi ya Taifa, akisisitiza kuwa jukumu la kulinda Tanzania ni la Serikali, vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla.

Katika mkutano huo, viongozi wa vyama vya siasa waliwasilisha maoni yao kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, huku Serikali ikiahidi kuendelea kuyapokea na kuyafanyia kazi kupitia mifumo rasmi ya majadiliano na maamuzi.

Mkutano huo uliowakutanisha wenyeviti, makamu wenyeviti, makatibu wakuu na viongozi wa jumuiya za vyama vya siasa nchini, ulikuwa wa pili wa aina hiyo kuitishwa na Rais Samia tangu kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Mkutano wa kwanza ulifanyika Machi 31, 2026, Ikulu jijini Dar es Salaam, ukiwakutanisha wagombea wa nafasi ya Urais na wagombea wenza kutoka vyama vya siasa vilivyoshiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

# Tamasha la Fahari 2026 kufungua milango ya biashara Zanzibar

**Bidhaa na huduma zinazozalishwa Zanzibar na Tanzania Bara zinatarajiwa kupata fursa mpya za masoko kupitia Tamasha la Fahari ya Zanzibar 2026, litakalofanyika kuanzia Septemba 4 hadi 14, 2026, kwa lengo la kutangaza uzalishaji wa ndani, kupanua masoko na kuimarisha uchumi.**

**Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEA), Juma Burhan, amesema hayo visiwani Zanzibar alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari. Amesema tamasha hilo litafanyika kwa mara ya tatu likiwa na kaulimbiu isemayo, “Bidhaa Zetu, Ndizo Fahari Yetu.”**

**Ameongeza kuwa tamasha hilo litatoa jukwaa kwa wazalishaji, wafanyabiashara na taasisi mbalimbali kuonesha bidhaa na huduma zao, huku likiwaunganisha wanunuzi, wawekezaji pamoja na wadau wa sekta mbalimbali kwa lengo la kukuza biashara na kuongeza ushindani wa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na Tanzania Bara.**

**Burhan amesema ufunguzi rasmi wa tamasha hilo utafanyika Septemba 5, 2026, ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi.**

**Aidha, amesema tamasha hilo linatarajiwa kuwa jukwaa la kubadilishana uzoefu, kujifunza mbinu mpya za biashara na kuhamasisha matumizi ya bidhaa za ndani, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha uchumi wa Zanzibar.**

صفر

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA MWANDISHI WETU

# Serikali yapokea boti mbili kuimarisha ulinzi na usalama wa bahari



Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba ameongoza hafla ya makabidhiano na uzinduzi wa boti mbili za kisasa za doria, Sailfish 2 na Sailfish 3, zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.6.

Boti hizo zitatumika kuimarisha ulinzi na usalama baharini na katika maziwa makuu nchini, ikiwa ni sehemu ya dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwekeza katika vifaa na teknolojia za kisasa zitakazoongeza uwezo wa taasisi husika kukabiliana na uhalifu na kulinda mipaka pamoja na rasilimali za Taifa kupitia maji.

Kila boti ina injini tatu zenye nguvu ya Horse Power (HP) 900, uwezo wa kwenda kwa kasi ya hadi noti 52, sawa na kilomita 96.3 kwa saa, urefu wa mita 12 na uwezo wa kubeba watu 12 kwa wakati mmoja.

Aidha, boti hizo zimefungwa vifaa vya usalama na uokoaji vitakavyowezesha utekelezaji wa operesheni kwa ufanisi katika mazingira mbalimbali ya bahari na maziwa.

Akizungumza wakati wa makabidhiano na uzinduzi wa boti hizo, uliofanyika Agosti 31, 2026 katika Bandari ya Dar es Salaam, Dkt. Mwigulu alizitaka Wizara na taasisi zinazohusika kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo ya boti hizo ili ziendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kudumu kwa muda mrefu.

Pia, amesisitiza kila Wizara na taasisi husika kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake, huku akiagiza kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya pande zote mbili za Muungano ili kuziba mianya inayoweza kutumiwa na wahalifu katika maeneo ya bahari na maziwa makuu.

Ameeleza kuwa ushirikiano wa karibu, uratibu madhubuti na matumizi sahihi ya teknolojia za kisasa ni nguzo muhimu katika kuimarisha usalama wa mipaka ya majini na kujenga mazingira salama yatakayochochea ukuaji endelevu wa uchumi wa buluu.



صفر

HABARI
MASHARIKI YA KATI

NA UKHTIFATIMA SS
0789 201 383



# Joto lafikia nyuzi 50 UAE, nchi 10 Mashariki ya Kati zaathirika

Joto limefikia nyuzi 50 Celsius katika Falme za Kiarabu huku takribani nchi 10 za Mashariki ya Kati zikikabiliwa na kipindi cha joto kali kinachotarajiwa kuendelea hadi wiki ijayo.

Kituo cha Taifa cha Hali ya Hewa cha UAE kilirekodi nyuzi 50 katika eneo la Al Shawamekh, Abu Dhabi, Jumamosi saa 8:30 mchana. Kwa mujibu wa Gulf News, hali kali zaidi inatarajiwa Kuwait, mashariki mwa Saudi Arabia, maeneo ya ndani ya UAE na Baghdad nchini Iraq.

Wataalamu wamesema joto hilo linasababishwa na mfumo mkubwa wa shinikizo la juu, unaojulikana kama "kuba la joto," unaozuia hewa ya moto kuondoka na kupunguza uwezekano wa mawingu kutanda.

Oman imerekodi hadi nyuzi 47.2 katika mji wa Bidiyah, huku Jordan ikitarajia viwango vya joto kupanda kwa nyuzi sita hadi nane juu ya wastani wa msimu.

Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Misri imetahadharisha kuwa unyevunyevu mkubwa unaweza kufanya joto la nyuzi 39 mjini Cairo lihisike kama nyuzi 42.

Mamlaka za afya zimewataka wananchi kuepuka shughuli nzito wakati wa mchana, kunywa maji ya kutosha na kutowaacha watoto au wazee ndani ya magari yaliyofungwa. Wafanyakazi wa nje, wazee na wenye matatizo ya kiafya wametajwa kuwa katika hatari zaidi.




MAKALA MAALUM

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Hafla za qasida aina hii zisinasibishwe na Uislamu

Katika miaka ya hivi karibuni kumeibuka hafla za usomaji wa qasida zilizopewa majina tofauti yenye mrengo wa Uislamu, jambo linalozifanya yanayofanyika humo kuchukuliwa kama ni sehemu ya mafundisho ya dini.

Hata hivyo, ni muhimu kutafakari kwa kina ikiwa mwenendo unaoshuhudiwa katika baadhi ya hafla hizo unaendana na maadili na misingi ya Uislamu au la.

Hakuna ubishi kwamba qasida au nasheed zina nafasi yake katika jamii ya Kiislamu pale zinapotumika kwa lengo la kuhimiza maadili mema, kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuwakumbusha Waislamu kuhusu dini yao.

Lakini kinachozua wasiwasi ni pale ambapo hafla za qasida zinapobadilika na kuwa matamasha ya miziki, huku zikiendelea kupewa sura ya kidini. Hali hii inaweza kuwachanganya watu na kuwafanya wadhani hayo ni katika mafundisho ya Uislamu.

Miongoni mwa mambo yanayozua maswali ni mchanganyiko usio na mipaka kati ya wanaume na wanawake, hali ambayo ni kinyume na mafundisho na maadili ya Kiislamu.

Tunaona wanawake wakitoka mbele ya wanaume na kwenda kumtunza au kumpa zawadi mwimbaji wa kiume hadharani. Bila kujali nia ya wahusika, matendo ya namna hii hayawiani na adabu na heshima ambazo Uislamu umeweka katika uhusiano kati ya wanaume na wanawake. Quran Tukufu imeweka miongozo inayolenga kulinda heshima, staha na maadili ya jamii, ikiwemo kuwataka Waumini wanaume na wanawake kushusha macho yao na kulinda heshima zao. Aidha, katika Suratul Ahzab na Suratul Nur kuna maelekezo yanayohimiza kujisitiri, kuwa na adabu na kuepuka mazingira yanayoweza kusababisha fitna.

Kwa msingi huo, ni wajibu wa Waislamu kuhakikisha kuwa shughuli zozote zinazohusishwa na dini zinazingatia maadili hayo badala ya kuyapuuza. Kinachoongeza uzito wa mjadala huu ni pale baadhi ya hafla hizi zinapohudhuriwa na watu tunaowaheshimu katika jamii, wakiwemo masheikh. Uwepo wao unaweza kuwafanya baadhi ya watu waamini kuwa kila kinachofanyika katika hafla hizo kimeidhinishwa na Uislamu.

Hata hivyo, ni muhimu kutenganisha heshima tuliyonayo kwa viongozi wetu na wajibu wa kutathmini matendo kwa mizani ya Quran na Sunna. Hakuna anayepaswa kuwa juu ya mafundisho ya dini.

## Mikusanyiko ya muziki

Baadhi ya hafla hizi hazina tofauti kubwa na mikusanyiko mingine ya wanamuziki isipokuwa majina yanayotumika na aina ya nyimbo zinazoimbwa.

Kunakuwa na shamrashamra, mapambo ya jukwaani, ushindani wa wasanii, utoaji wa zawadi kwa namna inayofanana na burudani nyingine, na wakati mwingine mazingira yasiyozingatia mipaka ya Kiislamu.

Ikiwa hali ndiyo hiyo, basi ni busara kutotumia dini kama nembo ya kuhalalisha shughuli, ambazo zinaweza kuwa na mambo yanayopingana na maadili yake.

Nisisitize hoja yangu si kupinga qasida wala kuwazuia watu kumtaja Mwenyezi Mungu kwa njia halali. Lengo ni kuhimiza tahadhari ili shughuli hizo zisipoteze mwelekeo na kugeuka kuwa burudani inayobeba jina la Uislamu bila kuakisi maadili yake.

Kila jambo linalofanywa kwa jina la dini linapaswa kuwa mfano wa uadilifu, staha na utiifu kwa mafundisho ya Qur'an na Sunna.

Wahusika wa hafla hizi wanapaswa kutafakari namna bora ya kuziendesha ili zisiwe chanzo cha malumbano na shubuha miongoni mwa Waislamu.

Ikiwa lengo ni kueneza mawaidha na maadili mema, basi mazingira ya hafla hizo yanapaswa kuonyesha maadili hayo kwa vitendo.

Heshima ya dini inalindwa si kwa majina ya hafla pekee, bali pia kwa mwenendo wa wanaoziratibu na wanaozihudhuria.

Kwa hiyo, kuna haja ya kutenganisha wazi kati ya shughuli za kijamii na mafundisho ya dini. Pale ambapo hafla zinakuwa na mienendo inayoweza kukinzana na maadili ya Kiislamu, si vyema kuzinasibisha moja kwa moja na dini yetu tukufu. Kufanya hivyo kunatia doa jina la Uislamu mbele ya jamii.

Waislamu wote tuna wajibu wa kulinda heshima ya dini yetu kwa kuhakikisha kwamba kila jambo linalofanywa kwa jina la Uislamu linaendana na mafundisho yake.

صَفَر

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Adui yetu mmoja, misimamo tofauti: Wito wa tafakuri mpya kwa Waislamu

Baada ya vita vya Marekani na Israel dhidi ya Iran kusimama kwa wiki kadhaa kupisha kile kinachoitwa "mazungumzo ya upatanishi", vita hivyo vimeanza tena hivi karibuni kufuatia mashambulizi makali ya makombora yaliyofanywa na Marekani katika maeneo mbalimbali ya Iran.

Shabaha ya mashambulizi hayo makubwa, ambayo yamesababisha uharibifu mkubwa, yalikuwa vituo vya kijeshi na miundombinu ya kiraia, kama vile barabara na madaraja. Rais wa Marekani, Donald Trump ameahidi kuvunja miundombinu yote ya Iran na kuirejesha nchi hiyo katika zama za kale, jambo ambalo ni uhalifu wa kivita.

Iran nayo inajibu mapigo kwa kushambulia vituo vya kijeshi vya Marekani vilivyopo katika eneo la Ghuba na Mashariki ya Kati, ikifanya mashambulizi ya makombora na ndege zisizo na rubani dhidi ya maslahi ya Marekani nchini Kuwait, Bahrain, Qatar, Jordan na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Inasikitisha kuona wananchi wa nchi zote hizo za Waislamu wakiishi katika taharuki na wasiwasi mkubwa kutokana na mashambulizi hayo yanayofanywa na Marekani na Iran.

Lakini jambo la kushangaza zaidi ni kuona kwamba Baraza la Ushirikiano la Nchi za Ghuba (GCC) likiilaani vikali Iran kwa kuzishambulia nchi za Ghuba. Baraza hili linatazama matukio haya kupitia macho ya Marekani na kutumia vipimo vilivyowekwa na taifa hilo la kibeberu.

GCC inayaona mashambulizi ya Iran dhidi ya Jordan, Bahrain, Qatar na Kuwait, lakini haioni kabisa ndege na makombora ya Marekani yakirushwa kutoka katika nchi hizo kuishambulia Iran. Inailaani Iran huku ikibaki kimya kuhusu nchi za Ghuba. Waislamu duniani tumefikia hatua ya hatari sana.

Umoja wa Nchi za Kiarabu (Arab League), Shirika la Ushirikiano wa Kiislamu (OIC) na Baraza la Ushirikiano la Nchi za Ghuba (GCC) vinaonekana kuanzishwa kama mbadala wa umoja wa Waislamu duniani, kufuatia kuporomoka kwa dola iliyowaunganisha Waislamu wote kuwa taifa moja bila kujali mipaka ya kijiografia.

Ni jambo la kushangaza na la ajabu kwamba hali isiyo ya kawaida imekuwa ikichukuliwa kuwa ya kawaida, na kile kisicho sahihi kimeanza kuonekana kuwa sahihi.

Nchi za Waislamu zimegawanywa na kuwa vidola vidogo dhaifu, hali ambayo si ya kawaida, lakini watu wengi wameifanya ionekane kuwa hali ya kawaida na sahihi.


Hali hii ya Waislamu haimpendezi Mwenyezi Mungu, Mtume wake wala waumini, kwa sababu ni hali iliyolazimishwa kwa Waislamu na wakoloni, kisha ikaendelezwa na viongozi wasio waadilifu katika nchi za Waislamu.


Vyombo vya habari vya Magharibi vinajaribu kupandikiza katika akili za Waislamu hali hii isiyo ya kawaida na kuifanya ionekane ya kawaida. Hili limewafanya Waislamu wengi duniani kusahau uhalisia wao kwamba wao ni Umma mmoja, vita yao ni moja, adui yao ni mmoja, amani yao ni moja, na wanapaswa kuongozwa na kiongozi mmoja.

GCC inapaswa kuyaangalia mambo kwa mtazamo wa Kiislamu zaidi na kutambua kwamba Marekani na mabeberu wengine ni maadui wa Uislamu na Waislamu, na kueleweka kwamba dola ya Kiyahudi ya Israel ni pandikizi lao katika ardhi ya Waislamu.

Jambo la ajabu ni hali hii isiyo ya kawaida ya Umma wa Kiislamu, ambao umegawanyika katika mataifa yenye watu wanaopingana na pengine hata kupigana. Mwenyezi Mungu anasema: "Hakika Waumini ni ndugu..." [Qur'an, 49:10].

Hivi sasa, nchi za Ghuba ya Uajemi na Mashariki ya Kati zinakabiliwa na mashambulizi ya Iran kujibu mashambulizi yanayofanywa dhidi yake, kwa sababu zimegeuzwa kuwa vituo muhimu vya Marekani, ambayo inatajwa kuwa adui namba moja wa Waislamu. Sasa ule udugu wa Kiislamu uliobainishwa na Mwenyezi Mungu katika Qur'an uko wapi, na kwa nini haupo?






# Mazishi ya Kiislamu: Ibada, Si Mila

## SEHEMU YA 1

**Kila jamii duniani ina utaratibu wake wa kuwazika wafu. Baadhi ya taratibu hizo zinatokana na dini, nyingine zinatokana na mila na desturi zilizorithiwa kizazi baada ya kizazi.**

Lakini kwa Muislamu, mazishi si jambo la kuachiwa mazoea ya jamii au hisia za watu. Ni sehemu ya ibada ambayo imewekewa mwongozo kamili na Allah Mtukufu kupitia Mtume Wake Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

Kwa masikitiko, katika sehemu nyingi za jamii zetu, taratibu za mazishi zimeanza kuchanganyika na mila za jadi, imani za kishirikina, au desturi zilizoathiriwa na dini nyingine.

Wakati mwingine watu hufanya mambo fulani kwa sababu tu: "Ndivyo tulivyowakuta wazee wetu wakifanya," bila kujiuliza kama yana msingi katika Qur'an na Sunna.

Hali hii imepelekea baadhi ya Sunna kusahaulika, huku desturi zisizo na dalili zikipewa uzito mkubwa. Matokeo yake ni kwamba wakati mwingine watu huona ni muhimu zaidi kutimiza mila za jamii kuliko kutekeleza mafundisho ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Allah Mtukufu amesema: "Na chochote anachokupeni Mtume, kichukueni; na anachokukatazeni, jiepusheni nacho." [Qur'an, 59: 7].

Aya hii inaweka msingi kwamba utiifu kwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) hauishii katika Swala, Saumu au Hija pekee, bali unahusisha pia namna ya kushughulika na maiti na kutekeleza mazishi.

Kadhalika, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwenye kufanya jambo ambalo halimo katika dini yetu, basi jambo hilo litakataliwa." [Bukhari na Muslim).

Hadith hii ni kanuni kubwa inayotukumbusha kuwa ibada zote zinapaswa kufanywa kwa kufuata mwongozo wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani). Mazishi nayo ni miongoni mwa ibada hizo. Mtu anapofariki, haki zake hazikatiki mara moja. Uislamu umeweka wajibu kwa walio hai kuhakikisha kuwa maiti anaoshwa kwa heshima, anavikwa sanda, anaswaliwa Swala ya Janaza, anazikwa kwa utaratibu wa Kisharia, na anaombewa dua. Haya yote ni haki ambazo Sharia imeziweka kwa Muislamu juu ya Waislamu wenzake.

Ndiyo maana Mtume (Allah amshushie rehema na amani) hakuliacha suala la mazishi bila mwongozo. Alifundisha namna ya kumhudumia anayekaribia kufa, namna ya kuosha maiti, namna ya kumvika sanda, namna ya kuswalia Janaza, namna ya kumzika, na hata dua zinazosemwa baada ya mazishi. Hii inaonesha kuwa mazishi ni sehemu ya ibada inayohitaji kufuata Sunna kama ilivyo katika ibada nyingine.

Lengo la mfululizo huu si kuwakosoa watu wala kuzusha mabishano. Lengo ni kurejea katika mwongozo wa Qur'an na Sunna kwa uelewa wa wanazuoni wa Ahlu Sunna wal-Jama'ah, ili kila Muislamu ajue nini anatakiwa kufanya anapokutana na msiba wa kufiwa.

Katika kila makala tutachambua hatua moja baada ya nyingine kuanzia dalili za Qur'an na Sunna, maelezo ya wanazuoni, makosa yanayojitokeza katika jamii, na namna ya kuyarekebisha kwa hekima. Tutagusia pia baadhi ya desturi zilizoenea ambazo hazina msingi wa Kisharia, ili kila mmoja aweze kutofautisha kati ya ibada na mila.

Tumuombe Allah Mtukufu atupe elimu yenye manufaa, atujaalie tuwe miongoni mwa wanaofuata Sunna ya Mtume Wake (Allah amshushie rehema na amani) katika maisha yetu na hata katika namna tunavyowazika wafu wetu. Hakika heshima ya maiti haipatikani kwa kufuata mila za watu, bali kwa kufuata mwongozo wa Allah na Mtume Wake (Allah amshushie rehema na amani).

Katika makala ijayo: Muislamu Anapokaribia Kufariki – Sunna zinazopaswa kufanywa kabla ya kifo kutokea.

KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Elimu zaidi itolewe kukabili homa ya ini

Maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani yalifanyika Julai 28, 2026, huku wito ukitolewa kwa wananchi kupima afya mara kwa mara ili kubaini ugonjwa mapema na kupata matibabu kwa wakati.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limesema homa ya ini inaendelea kuwa tishio kubwa kwa afya ya jamii duniani kutokana na ukosefu wa elimu sahihi na uzembe wa kuchukua tahadhari.

Kwa mujibu wa WHO, kila baada ya sekunde 30 mtu mmoja hufariki dunia kutokana na magonjwa yanayohusiana na homa ya ini. Aidha, virusi vya Hepatitis B na Hepatitis C husababisha takribani vifo milioni 1.3 kila mwaka duniani.

Hali hii inaashiria kuwa homa ya ini ni ugonjwa uliosahaulika, lakini bado ni tishio kubwa kwa jamii.

## Tahadhari ya maradhi katika Uislamu


Katika Uislamu, kulinda afya kwa kuchukua tahadhari stahiki ni sehemu muhimu ya maisha ya kila siku. Dini ya Kiislamu inahimiza matumizi ya njia halali na salama za kujikinga na maradhi, ikiwemo chanjo.

Kupata chanjo si ishara ya udhaifu wa imani, bali ni kutumia sababu ambazo Mwenyezi Mungu amezijaalia ili kuzuia maambukizi ya magonjwa mbalimbali kabla hayajasababisha madhara makubwa.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatwambia: "...wala msijiangamize kwa mikono yenu wenyewe..." [Qur'an, 2:195]. Vilevile, Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) ametuhimiza kujikinga na maradhi aliposema: "Hakuna kujidhuru wala kusababisha madhara." [Ibn Majah].

Mafundisho haya yanaweka msingi wa kulinda afya ya mtu binafsi na ya jamii kwa kuchukua tahadhari zinazoweza kuwakinga dhidi ya maradhi. Hivyo, ni muhimu kila mmoja kuchukua hatua kwa kupima afya mara kwa mara na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya ili kujikinga dhidi ya maambukizi.

Mapambano dhidi ya homa ya ini yanahitaji msukumo mkubwa zaidi kutoka serikalini, kwa wataalamu wa afya na wananchi kwa ujumla. Viongozi wa dini pia wana nafasi muhimu ya kutumia majukwaa yao kuhamasisha waumini kulinda afya kama sehemu ya kutekeleza mafundisho ya dini.




Kwa hakika, ushindi dhidi ya homa ya ini utapatikana pale kila mmoja atakapotekeleza wajibu wake. Kinga ndiyo silaha muhimu zaidi katika mapambano dhidi ya homa ya ini.

Elimu kuhusu njia za maambukizi, umuhimu wa chanjo, matumizi salama ya vifaa vya matibabu na umuhimu wa uchunguzi wa afya wa mara kwa mara inapaswa kupewa kipaumbele ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu ugonjwa huu.

Aidha, jamii inapaswa kuachana na imani potofu zinazowafanya baadhi ya watu kuchelewa kupima afya au kutafuta matibabu. Bila kuchukua hatua madhubuti za kinga, gharama za matibabu na athari za homa ya ini zitaendelea kuongezeka.

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Sababu Marekani kutaka kudhibiti Mlango-Bahari wa Hormuz




Siku chache zilizopita, Rais wa Marekani, Donald Trump alitangaza kwamba Marekani itatoza ada ya asilimia 20 kwa bidhaa zote zinazosafirishwa kupitia Mlango–Bahari wa Hormuz kufuatia uzinduzi wa operesheni maalumu ya kijeshi iliyowasha upya vita katika Ghuba ya Arabia.

Kujibu tangazo hilo la Trump, Shirika la Kimataifa la Bahari (IMO), ambalo ni taasisi ya Umoja wa Mataifa, lilithibitisha tena msimamo wake wa kupinga utozwaji wa ada za usafiri katika njia yoyote inayotumika kwa usafirishaji wa kimataifa, likisisitiza kuwa hatua hiyo ni kinyume cha sheria.

Ni wazi kwamba hakuna mantiki yoyote nyuma ya maamuzi ya Trump zaidi ya kiburi, majivuno, dharau kwa utajiri wa Waislamu na kupuuza usalama wa ardhi zao.

Kwa hakika, Marekani yenyewe ndiyo iliyoanzisha vita hivi na kuvilazimisha kwa watu wa eneo hilo. Imefanya mashambulizi ya mabomu, imeua watu, imeharibu majengo na miundombinu, na kuchoma moto maeneo kadhaa nchini Iran.

Sasa imezivuta nchi za eneo zima la Ghuba na Mashariki ya Kati katika mzingiro wa mapambano ya kijeshi, ambayo lengo lake linalotangazwa sasa limekuwa kufungua tena Mlango–Bahari wa Hormuz, ingawa mlango huo ulikuwa wazi hapo awali kabla ya mashambulizi ya Marekani nchini Iran!

Badala ya kuomba msamaha kwa watu wa eneo hilo na ulimwengu mzima kwa uharibifu mkubwa iliyoufanya, na badala ya kulipa fidia kwa hasara za kiuchumi katika masoko ya kimataifa zilizosababishwa na Marekani, Rais Trump sasa anadai malipo kwa ajili ya kuufungua tena Mlango–Bahari wa Hormuz na kuhakikisha usalama wake!

Hali hii inaakisi dharau ya Marekani kwa Waislamu na kiwango cha kiburi kilichomgubika Rais Donald Trump, kiasi cha kuifanya Marekani ionekane kuwa na haki ya kunyakua utajiri wa mataifa mengine.

Hii si mara ya kwanza kwa Rais Trump kuzungumzia nchi tajiri, akimaanisha mataifa ya Ghuba, kwamba yailipe Marekani fedha. Hapo awali, alidai mataifa hayo yabebe gharama zote za vita vya Marekani dhidi ya Iran. Trump anawachukulia watawala wa nchi za Ghuba kana kwamba wao ni pochi zilizo mfukoni mwake!

Iwapo Trump atafanikiwa kutekeleza maono yake katika eneo la Ghuba na Mashariki ya Kati, hiyo itakuwa aibu kubwa zaidi kwa Waislamu duniani, kwa sababu mustakabali wa eneo hilo pamoja na rasilimali zake utakuwa chini ya udhibiti wa mabeberu kutoka nje.

Watawala wa eneo hilo wanaoshirikiana na Trump, ikiwa ni pamoja na kuruhusu uwepo wa kambi za kijeshi za Marekani zinazotumika kutekeleza operesheni za kijeshi zinazolenga kulidhoofisha eneo hilo, ni sawa na watu wanaoelekea kwenye maangamizi yao wenyewe. Hii ni hasara kubwa zaidi!

Allah anasema: "Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale waliokupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanaowafanya hao marafiki basi hao ndiyo madhalimu." [Qur'an, 60:9].

Matukio yanayoendelea sasa yanatoa fursa kwa nchi za Ghuba kujinasua kutoka katika kivuli cha Marekani. Marekani haipo tena katika nafasi yake ya awali ya nguvu na ushawishi, huku ikitambua kupungua kwa uwezo wake kutokana na changamoto mbalimbali zinazoikabili.

Marekani imepoteza marafiki na washirika wake, nguvu ya washindani wake wa kimataifa kama vile China na Urusi imeongezeka, wananchi wake hawataki kubeba gharama za vita, na imefilisika kifikra na kiustaarabu.

Na Said Rajab
0783 650 803

صفر

# Umuhimu wa mazungumzo katika kudumisha amani



## SEHEMU YA 2 YA MWISHO

**Katika kuhitimisha makala haya kuhusu nafasi ya mazungumzo katika kudumisha amani, leo tunaangazia umuhimu wa kuondoa wingu la tuhuma na shaka linaloweza kuwafanya watu kuhoji kimakosa hamasa, nia na heshima za wengine.**

Imepokewa kuwa bedui mmoja alimjia Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) na kusema: "Mke wangu amejifungua mtoto wa kiume mwenye rangi nyeusi, nami nimemkataa." Mtume wa Mwenyezi Mungu akamuuliza: "Je, una ngamia?" Akajibu: "Ndiyo." Mtume akauliza: "Wana rangi gani?" Bedui huyo akajibu: "Nyekundu."

Mtume akauliza tena: "Je, kuna ngamia wa rangi ya kijivu miongoni mwao?" Akajibu: "Hakika, wapo."

Mtume akauliza: "Unafikiri hilo limetokeaje?" Bedui huyo akajibu: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, huenda ni kutokana na asili ya ukoo wao." Mtume akasema: "Huenda mtoto huyu pia ametokana na asili kama hiyo." Hivyo Mtume hakumruhusu bedui kumkataa mtoto huyo. [Bukhari na Muslim].

Mazungumzo hayo yalifanikiwa kuondoa tuhuma na mawazo mabaya yaliyokuwa yamemjia mwanaume huyo dhidi ya mkewe, hivyo kukata mizizi ya shaka na kufunga mlango wa kutoelewana katika familia.

Mazungumzo huwa na athari kubwa pale yanapoendeshwa na mtu mwenye ujuzi, utulivu, anayelenga kufikia ukweli, anayeongozwa na uadilifu, na aliye mbali na kukashifiana au kuzua mabishano yasiyo na tija.

Katika suala la malezi ya watoto, mazungumzo yana nafasi kubwa zaidi kuliko kutoa amri pekee au kulazimisha mambo bila maelezo. Wakati mmoja, Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani zimshukie) alimwona Hassan bin Ali (Allah amridhie) akiweka kinywani mwake tende ya sadaka.

Mtume akasema: "Khakh" (usemi wa kukataza)! Hivi hujui kwamba sisi hatuli kile kinachotolewa kwa ajili ya sadaka?" [Bukhari hadith namba 3072; na Muslim hadith namba 1069].

Hakika malezi yanayoambatana na kueleza mantiki na hekima huwa bora zaidi kuliko malezi yanayotegemea amri bila ufafanuzi. Kama kukataza pekee kungetosha katika malezi, basi Mtume angeishia kusema "Khakh" tu. Lakini kuongeza mazungumzo na kutoa hoja kulimsaidia Hassan kupata uelewa sahihi, badala ya kulazimishwa kufuata jambo bila kufahamu sababu yake.

Jamii yoyote inayojenga uwezo wa kuwasilisha mawazo kwa ushawishi kupitia mazungumzo, uwazi na mijadala yenye heshima huwa ni jamii iliyostaarabika. Hii ni kwa sababu jamii hiyo huwasilisha mawazo kwa uwazi, kwa uelewa sahihi na kwa unyenyekevu, badala ya kiburi.

Hata kama matokeo hayatakuwa kama yalivyotarajiwa, angalau ukweli utakuwa umewekwa bayana na watu watakuwa wametimiza wajibu wao. Hili linadhihirishwa na kauli ya Waumini iliyonukuliwa katika Qur'an: "Basi mtayakumbuka ninayokuambieni, na mimi namkabidhi Mwenyezi Mungu mambo yangu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaona waja wake." [Qur'an, 40:44].

NA UKHTIFATIMA SS
0789 201 383

# Hamas kukubali kukabidhi silaha: Mwanzo wa mwisho wa mgogoro?

Kwa karibu miaka 40, Hamas imejieleza kama harakati ambayo siasa na mapambano ya silaha haviwezi kutenganishwa. Sasa, kwa mara ya kwanza tangu vita vya sasa vya Gaza vianze, kundi hilo limekubali mpango unaoweza kulifanya liweke chini silaha zake nzito.

Hili ni badiliko kubwa—lakini si kujisalimisha.

Hamas inasema iko tayari kuweka silaha zake nzito chini ya mamlaka ya chombo kipya cha utawala wa Kipalestina. Mahandaki, maghala na maeneo ya kutengeneza silaha yatatambuliwa, kufungwa au kuharibiwa.

Israel nayo inatakiwa kuondoa majeshi yake Gaza hatua kwa hatua, huku kikosi cha kimataifa kikisimamia usalama na utekelezaji.

Kwa lugha rahisi, mpango unasema: Hamas iondolewe uwezo wa kijeshi, Israel iondoke, halafu Gaza itawaliwe na kamati ya wataalamu wa Kipalestina badala ya jeshi la Israel au utawala wa Hamas.

Lakini hapo ndipo tatizo linaanzia. Hamas haitaki kuanza mchakato huo kabla Israel haijasitisha mashambulizi, kuondoa majeshi na kuruhusu misaada kuingia. Israel nayo haitaki kuondoka kabla haijathibitisha kuwa Hamas imeondolewa uwezo wa kupigana.

Ni kama watu wawili waliogeuziana bunduki huku kila mmoja akisema: "Wewe ndiye uanze kuiweka chini."

Mpango unataka hatua hizo zifanyike sambamba. Hamas inapoweka silaha chini, Israel nayo iondoe majeshi katika maeneo yaliyokubaliwa. Kila hatua ithibitishwe kabla ya kuingia nyingine.

## Mpango wa Trump ulipoanzia

Makubaliano haya hayajaibuka ghafla. Ni awamu ya pili ya mpango wa vipengele 20 wa Rais Donald Trump, uliotangazwa Septemba 2025. Awamu ya kwanza ilileta usitishaji mapigano Oktoba, kubadilishana mateka na wafungwa, kuongeza misaada na kuondoka kwa sehemu ya majeshi ya Israel hadi eneo linaloitwa "Mstari wa Njano."

Lakini maswali magumu yaliachwa wazi: Hamas itafanya nini na silaha zake, Israel itaondoka lini na nani ataitawala Gaza?

Marekani ndiyo injini ya mpango huu. Trump ameunda Baraza la Amani kusimamia utekelezaji, utawala wa mpito na ujenzi wa Gaza. Misri, Qatar na Türkiye zimekuwa wapatanishi wakuu, huku Misri na Jordan zikisaidia kuwafundisha polisi wapya wa Kipalestina.

Kamati ya Kitaifa ya Utawala wa Gaza, inayoundwa na wataalamu wa Kipalestina, inatarajiwa kuchukua utawala wa kila siku. Kwa mujibu wa BBC, kamati hiyo bado haijaingia Gaza na imekuwa ikifanya kazi kutoka Cairo. Kikosi cha Kimataifa cha Kuleta Utulivu nacho kinatarajiwa kusaidia polisi wa Kipalestina kuchukua majukumu ya usalama.

## Historia ya mzozo

Vita vya sasa vililipuka Oktoba 7, 2023, baada ya Israel kudai Hamas imeshambulia kusini mwa Israel, na kuua zaidi ya watu 1,200 na kuwateka zaidi ya 250. Israel ilijibu kwa vita vilivyoharibu sehemu kubwa ya Gaza, kuua makumi ya maelfu ya Wapalestina na kuacha zaidi ya watu milioni mbili katika mazingira mabaya.

Lakini mgogoro haukuanza hiyo Oktoba 7.

Mwaka 1948 ulishuhudia kuundwa kwa Israel na Nakba—kufurushwa au kukimbia kwa mamia ya maelfu ya Wapalestina. Mwaka 1967, Israel iliikalia Gaza, Ukingo wa Magharibi na Jerusalem Mashariki.

Hamas ilianzishwa mwaka 1987, ikashinda uchaguzi wa Palestina mwaka 2006 na kuchukua udhibiti wa Gaza mwaka uliofuata. Israel ikaweka kizuizi, na Gaza ikaingia katika mizunguko ya mashambulizi, vita na majanga ya kibinadamu.

## Kwa nini Hamas imebadilika sasa?

Gaza imeharibiwa, raia wamechoka na Hamas imepoteza viongozi wengi pamoja na sehemu ya uwezo wake wa kijeshi. Nchi za Kiarabu na wafadhili sasa wanataka kuzungumzia ujenzi na utawala, si vita visivyo na mwisho.

Kukabidhi silaha kwa chombo cha Kipalestina—badala ya Israel—kunaweza kuipa Hamas njia ya kuacha jukumu la kijeshi bila kutangaza kuwa imesalimu amri.

Kwa Israel, hilo linaibua swali gumu. Ikiwa lengo lake lilikuwa kuondoa silaha na utawala wa Hamas, je, itakubali kuondoka masharti hayo yakitekelezwa?

Kwa sasa, makubaliano bado yako kwenye karatasi. Israel haijayakubali wazi, mrengo mkali serikalini unaypinga na utaratibu kamili wa utekelezaji haujakamilika.






UKHTI FATIMA SS

# Waislamu wahimizwa kuhakiki bidhaa za halal




Waislamu Afrika ya Mashariki wamehimizwa kutotegemea nembo ya halal pekee, bali kuchunguza viambato, chanzo cha bidhaa na uhalali wa taasisi iliyotoa cheti.

Wito huo umetolewa katika Kongamano la Halal la Afrika Mashariki lililofanyika Nairobi, likiwakutanisha watunga sera, wasafirishaji, mashirika ya uthibitishaji na wafanyabiashara kujadili nafasi ya Kenya katika soko la kimataifa la halal, kwa mujibu wa tovuti ya Eastleighvoice

Katibu Mkuu wa Taasisi ya Viwango na Metrolojia ya Nchi kwa ajili ya nchi za Kiislamu, İhsan Övüt, amesema uhalali wa bidhaa hauishii katika namna ya kuchinja, bali unahusisha pia viambato, uchakataji, ufungashaji na viwango vya ubora. Aliwataka watumiaji kusoma maelezo ya bidhaa na kuthibitisha uaminifu wa nembo wanazokutana nazo.

Mtaalamu wa uthibitishaji wa halal, Hamisi Mgeni, amesema baadhi ya biashara katika maeneo yenye Waislamu wengi bado hazina vyeti rasmi, jambo linaloweza kuwafanya walaji kuamini bidhaa kwa mazoea badala ya ushahidi.

Amesema umiliki wa biashara na Muislamu pekee si uthibitisho wa halal, kwa kuwa chanzo cha nyama na viambato kinaweza kutokidhi viwango vinavyotambuliwa.

Wajumbe pia wametaka Kenya iwe na mfumo wa kitaifa wa halal, viwango vinavyolingana na usimamizi madhubuti ili kuongeza imani ya walaji na kurahisisha mauzo katika masoko ya kimataifa.

# 35 wachunjwa ujumbe Tume ya Wakfu Kenya

**Mchakato wa kuwapata wajumbe wa Tume ya Wakfu nchini Kenya umeingia hatua mpya baada ya jopo la uteuzi kutangaza majina ya wagombea 35 waliochaguliwa kuendelea na mchakato huo.**

**Jopo hilo, linaloongozwa na Sheikh Ibrahim Lethome Asmani, lilisema lilipokea maombi 148 kwa nafasi nane zilizotangazwa. Wagombea walioingia kwenye orodha hiyo wanatoka kaunti mbalimbali, zikiwamo Mombasa, Wajir, Lamu, Kilifi, Mandera, Garissa, Nairobi, Kwale na Taita Taveta.**

**Jamii ya Waislamu nchini humo imepewa siku 14 kuwasilisha kwa maandishi taarifa zozote muhimu kuhusu wagombea hao. Taarifa hizo zinaweza kuwasilishwa kwa jopo kupitia ofisi yake jijini Nairobi au kwa baruapepe iliyotolewa. Mawasilisho ya nakala ngumu yanatakiwa kufungwa na kuwekwa alama ya siri.**

**Jopo limeeleza kuwa linaweza kumhoji mtu yeyote atakayewasilisha taarifa kuhusu mgombea kabla ya kufanya mapendekezo ya mwisho.**

**Tume ya Wakfu ina jukumu la kusajili, kusimamia na kulinda mali zilizowekwa wakfu kwa shughuli za kidini, kijamii na misaada. Chini ya Sheria ya Wakfu ya mwaka 2022, tume hiyo pia inapaswa kuhakikisha mali hizo zinatumika kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia sheria.**

**Baada ya usaili, majina yatakayopendekezwa yatawasilishwa kwa Waziri wa Ardhi na Mipango kwa ajili ya uteuzi.**

UKHTI FATIMA SS




# Ethiopia kuandaa kongamano la huduma za fedha zisizo na riba




Ethiopia itaandaa Kongamano la Sita la Kimataifa la Benki Zisizo na Riba na Takaful pamoja na tuzo za sekta hiyo, Agosti 17, mwaka huu, katika Hoteli ya Hyatt Regency jijini Addis Ababa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kituo cha AlHuda cha Benki na Uchumi wa Kiislamu, chenye makao yake Umoja wa Falme za Kiarabu, kongamano hilo litafanyika chini ya udhamini wa Benki Kuu ya Ethiopia.

Waandaaji wamesema mkutano huo utawakutanisha wasimamizi wa fedha, watunga sera, wanazuoni wa Sharia, wawekezaji na taasisi za kifedha kutoka Afrika, Mashariki ya Kati, Asia na Ulaya.

Mkurugenzi Mtendaji wa AlHuda, Muhammad Zubair Mughal, amesema kongamano na tuzo hizo zinalenga kutambua taasisi na wataalamu waliochangia uvumbuzi, uongozi na maendeleo ya huduma za fedha zisizo na riba.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mijadala itahusu benki zisizo na riba, takaful, teknolojia za kifedha, mikopo midogo, usimamizi wa Sharia na ujumuishaji wa kifedha. Tuzo zitatolewa katika maeneo mbalimbali, yakiwamo benki, takaful, teknolojia za kifedha na miradi ya uwezeshaji wa wanawake.

Waandaaji wameeleza kuwa muda wa kuwasilisha majina ya wanaowania tuzo utafungwa Agosti 10, kabla ya maombi kupitiwa na jopo la wataalamu, wasomi na wanazuoni wa Sharia.

# Cambodia yazindua kampeni ya kitaifa ya ithbati ya halal

**Serikali ya Cambodia imezindua kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha na kurahisisha usajili wa vyeti vya halal, hatua inayolenga kuongeza ushindani wa bidhaa za ndani na kuzifungulia biashara masoko ya halal nchini na kimataifa.**

**Kampeni hiyo inaendeshwa na Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na Kamati ya Ukaguzi wa Bidhaa za Halal ya Cambodia. Waziri wa Biashara, Cham Nimul, amesema mpango huo utawezesha wazalishaji kufahamu viwango vinavyotakiwa na kutumia nembo rasmi ya halal kwa kufuata taratibu.**

**Mabadiliko yaliyotangazwa yanajumuisha kupunguza muda wa kushughulikia maombi kutoka siku 90 hadi siku 60 za kazi. Uhalali wa cheti umeongezwa hadi miaka miwili, huku waombaji binafsi wakiruhusiwa kujisajili na bidhaa zaidi kuingizwa katika mfumo wa uthibitishaji.**

**Serikali pia inalenga kuongeza uelewa miongoni mwa wafanyabiashara kuhusu faida za viwango vya halal na tahadhari dhidi ya matumizi yasiyo halali ya nembo hiyo.**


**Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza thamani ya bidhaa zinazotengenezwa Cambodia na kuimarisha uwezo wa kampuni za ndani kushindana katika soko la kimataifa la halal.**

**Kampeni hiyo imehusisha wizara, taasisi za serikali, vyama vya wafanyabiashara, kampuni na wawakilishi wa Mpango wa Kijiji Kimoja, Bidhaa Moja.**

# Kuweka Kimkakati

## Waqf na uchumi wa maarifa – mtaji wa taifa la kesho

**Leo, utajiri na ushindani wa mataifa hautegemei tena mafuta, dhahabu, madini au ardhi yenye rutuba pekee, bali unategemea maarifa, utafiti, ubunifu na uwezo wa watu wake kuzalisha suluhisho jipya kwa changamoto zinazowakabili.**




Mataifa yanayoongoza duniani yamewekeza kwa nguvu katika elimu, sayansi na teknolojia, na matokeo yake yamekuwa ukuaji wa uchumi unaotegemea akili na ubunifu kuliko maliasili.

Makala hii ni muendelezo wa kuangaza umuhimu wa kuwekeza kwenye elimu na maarifa adimu

Makampuni makubwa duniani yanathaminiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na maarifa, uvumbuzi na uwezo wa wataalamu wake kuliko thamani ya majengo au vifaa vinavyomilikiwa. Teknolojia za akili unde (Artificial Intelligence), tiba za kisasa, nishati mbadala, fedha za kidijitali, kilimo cha kisasa na usalama wa mtandao ni baadhi ya sekta zinazounda uchumi wa kesho. Hivyo, taifa lenye wataalamu wengi na mazingira yanayochochea ubunifu ndilo lenye nafasi kubwa ya kufanikiwa.

Swali muhimu la kujiuliza ni hili: Je, taasisi zetu za Waqf zina nafasi gani katika kujenga uchumi huu wa maarifa?

Jibu ni kwamba zina nafasi kubwa sana. Kwa historia yake, Waqf imekuwa nguzo ya maendeleo ya elimu, afya na ustaarabu wa Kiislamu.

Vyuo vikuu, maktaba, hospitali na vituo vya utafiti vilivyofadhiliwa kwa Waqf vilichangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sayansi na maarifa katika ulimwengu wa Kiislamu kwa karne nyingi. Leo, kuna haja ya kufufua dhima hiyo kwa mtazamo unaoendana na mahitaji ya zama hizi. Badala ya kusubiri serikali pekee kugharamia elimu ya juu, tafiti na uvumbuzi, taasisi za Waqf zinaweza kutumia mali na rasilimali zake kuanzisha vituo vya utafiti, kufadhili wanafunzi wa shahada za uzamivu, kusaidia wabunifu vijana, kuanzisha maabara za kisasa na kuwezesha ushirikiano kati ya vyuo vikuu, sekta binafsi na taasisi za kimataifa.

Hatua hizi, zitasaidia kuzalisha maarifa mapya, kuongeza ajira zenye tija na kujenga kampuni za teknolojia zinazomilikiwa na wazawa.

Katika mtazamo wa Maqaswid ash-Shari'ah, uwekezaji wa aina hii unalinda maslahi ya umma kwa kuimarisha uchumi, kuhifadhi mali, kuendeleza elimu na kuongeza uwezo wa jamii kujitegemea. Waqf inayowekeza katika maarifa haijengi mtu mmoja tu, bali hujenga kizazi kizima chenye uwezo wa kuleta mabadiliko ya kudumu.

Waqf ya leo haipaswi kuangalia mahitaji ya sasa pekee. Inapaswa kuandaa taifa kwa miaka 30 au hata 50 ijayo.

Ikiwa hatutaanza sasa kuwekeza katika wataalamu wa akili unde (AI), usalama wa mtandao, bioteknolojia, sayansi ya anga, robotiki, uchambuzi wa data, teknolojia ya nishati na taaluma nyingine zinazoibuka, tutaendelea kuwa watumiaji na wanunuzi wa teknolojia zinazotengenezwa na wengine badala ya kuwa wabunifu na wazalishaji wake.

Kwa hiyo, Waqf inaweza kuwa daraja linalounganisha ibada na maendeleo ya taifa. Kila mwanafunzi anayefadhiliwa, kila mtafiti anayesaidiwa, kila maabara inayojengwa na kila uvumbuzi unaozaliwa kupitia Waqf ni sadaka yenye manufaa yanayoendelea na wakati huo huo ni uwekezaji wa kimkakati unaoongeza nguvu ya uchumi wa taifa.

NA UKHTI FATIMA



# Fikra 7 potofu kuhusu huduma za fedha za Kiislamu

**Huduma za fedha za Kiislamu zinaendelea kupanuka katika nchi za Kiislamu na zisizo za Kiislamu. Hata hivyo, watu wengi bado huzitazama kwa mashaka kutokana na taarifa zisizo sahihi, kutofahamu mikataba yake au kulinganisha mwonekano wa bidhaa zake na ule wa benki za kawaida. Hizi ni fikra saba zinazojirudia na ukweli wake.**

### *Mosi:* Benki za Kiislamu zinap'naswa kutoa fedha bure

Kukataza riba hakumaanishi benki ya Kiislamu ni taasisi ya kutoa fedha bure. Uislamu umeruhusu biashara na faida halali, lakini umekataza riba. Kwa hiyo, taasisi hizi hupata mapato kupitia mikataba kama murabaha, yaani kuuza mali kwa bei inayojumuisha faida inayojulikana; ijara, au upangishaji; na musharakah na mudarabah, zinazohusisha ubia na mgawanyo wa faida.

Tofauti kuu ni kwamba mapato yanapaswa kutokana na biashara, mali au uwekezaji halisi, si kuongeza fedha juu ya mkopo kwa sababu ya muda pekee.

### *Pili:* Ni benki za kawaida zilizobadilishiwa majina ya Kiarabu

Bidhaa za Kiislamu zinaweza kufanana kwa nje na za kawaida: zina akaunti, kadi, malipo ya kila mwezi na ufadhili wa nyumba au biashara. Hata hivyo, uhalali wake hautegemei jina, bali muundo wa mkataba, umiliki wa mali, mgawanyo wa hatari na shughuli inayofadhiliwa.

Taasisi inayodai kufuata Sharia inanpaswa kuwa na usimamizi wa kitaalamu wa Sharia na taratibu za ukaguzi. Hata hivyo, wateja hawapaswi kuridhika na lebo pekee; wanapaswa kusoma mkataba na kuuliza namna faida, gharama na hatari zinavyohesabiwa.

### *Tatu:* Huduma hizi ni za Waislamu pekee

Fedha za Kiislamu zimejengwa juu ya kanuni za uwazi, uadilifu, uwajibikaji na uhusiano wa fedha na shughuli halisi za kiuchumi. Kanuni hizi si mali ya waumini wa dini moja.

Ndiyo maana watu na serikali zisizo za Kiislamu – Ulaya, Amerika na kwingineko - zimewahi kutumia na bado zinatumia sukuk na bidhaa nyingine za Kiislamu kuvutia wawekezaji na kugharamia miradi. Mteja asiye Mwislamu anaweza kutumia huduma hizo endapo anakubaliana na masharti yake.

### *Nne:* Sharia inahusu kuepuka riba na pombe tu

Kufuata Sharia ni pana kuliko kuondoa riba au kukataa kufadhili pombe na kamari. Kunahusisha pia kuzuia udanganyifu, masharti yasiyoeleweka, dhuluma, ubashiri uliopitiliza na biashara zisizo na mali au shughuli halisi.

Pia kunasisitiza haki katika mikataba, uwazi wa gharama na uwajibikaji wa pande zote. Vyombo kama zakat, wakfu na qard al-hasan, yaani mkopo mwema usio na riba, vinaweza kuunganisha huduma za fedha na ustawi wa jamii.

### *Tano:* Fedha za Kiislamu ni za zamani na zinapinga teknolojia

Hakuna kanuni ya Kiislamu inayokataza teknolojia kwa sababu tu ni mpya. Kinachopimwa ni matumizi yake, madhara yake na uhalali wa mkataba.

Ndiyo maana kuna benki za kidijitali, majukwaa ya uwekezaji, ufadhili wa pamoja, sukuk za kidijitali na huduma za fedha kupitia simu zinazolenga kufuata Sharia. Changamoto si kukubali kila uvumbuzi, bali kuhakikisha kasi ya teknolojia haizidi uwezo wa udhibiti na ulinzi wa mteja.

### *Sita:* Mchakato wake ni mgumu kuliko benki za kawaida

Istilahi kama murabaha, ijara na musharakah zinaweza kumchanganya mteja mpya. Lakini ugumu mara nyingi unatokana na kutokuzoea lugha hiyo, si lazima mchakato wenyewe.

Taasisi yenye uwazi inapaswa kueleza kwa lugha rahisi nani anamiliki mali, nani anabeba hatari, malipo yanahesabiwaje na nini hutokea mteja akichelewa kulipa.

### *Saba:* Huduma za Kiislamu daima ni ghali zaidi

Baadhi ya bidhaa zinaweza kuwa ghali kutokana na gharama za kisheria, kodi, ukaguzi wa Sharia au soko dogo. Lakini si sahihi kusema bidhaa zote ni ghali kila wakati.

Gharama hutofautiana kulingana na taasisi, nchi, bidhaa na ushindani wa soko. Mteja anapaswa kulinganisha jumla ya malipo, ada, masharti ya kuchelewa na hatari, si kuangalia kiwango cha faida pekee.

Fedha za Kiislamu si mfumo mkamilifu usioweza kukosolewa. Ubora wake hutegemea kama kanuni zake zinatekelezwa kwa uaminifu. Suluhisho si kuamini kila bidhaa yenye jina la Kiislamu, wala kuikataa kwa sababu ya mwonekano wake, bali kuichunguza kwa maarifa, mkataba na ushahidi.

صفر فتاوى

# Je, kazi ya uwakili ni halali?



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

## *Swali:* Nini hukumu ya Uislamu kuhusu kazi ya uwakili? Je, ni halali au haramu? Na je, uwakili ulikuwepo katika Uislamu?

***Jawabu:*** Uwakili (kumsimamia mtu katika kesi ya madai dhidi ya mwingine) ni aina ya uwakala, jambo ambalo lipo katika Uislamu kwa ushahidi wa Qur'an na Sunna.

Uwakala katika migogoro na kesi ni sehemu ya uwakala.

Ikiwa wakili anayemuwakilisha mtu katika kesi analenga kutetea haki, kuondoa batili, na kumpa kila mwenye haki haki yake, basi uwakili huo hauna tatizo, bali unaweza kuwa ni wema kwa yule asiyefahamu namna ya kujitetea.

Ndiyo maana Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisema: "Mnakosana mbele yangu, na huenda baadhi yenu akawa mahiri katika hoja zake kuliko mwingine. Mimi ninamhukumia kulingana na ninachosikia. Basi, yeyote ambaye nimemhukumia kitu kilicho haki ya ndugu yake, basi ajue nimemkatia kipande cha moto wa Jahannam, akae nacho au akiachilie." [Bukhari na Muslim].

Lakini ikiwa wakili analenga tu kushinda kesi kwa niaba ya mteja wake, iwe ni kwa haki au kwa batili, basi hilo halijuzu katika Uislamu.

Uwakala wa aina hiyo ni haramu, na kila pesa anayochukua kwa uwakili huu ni haramu, kwa sababu ni katika kusaidia batili. Mwenyezi Mungu amesema: "Na saidianeni katika wema na taqwa, wala msisaidiane katika dhambi na uadui." Rejea Surat Al-Maida aya ya: 2

Hivyo uwakili una mambo mawili. Kama ni kwa ajili ya haki →halali, na kama ni kwa ajili ya batili →haramu. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## *Swali:* Mtu anayefanya kazi kama wakili wakati mwingine hutetea mwenye kudhulumu., huku akijitetea kuwa "Hii ndiyo kazi yangu." Je, katika Uislamu kuna uwakili (advocacy)?

***Jawabu:*** Uwakili una hatari kubwa. Uwakili ni uwakilishi wa yule anayempa kazi ya kumuwakilisha.

Iwapo wakili anajitahidi katika kutafuta haki, anatetea haki, na anajitahidi kuhakikisha haki inafika kwa mwenye haki, na haimbebi kuwa wakili kiasi cha kumsaidia mwenye kudhulumu, au kuwapotosha mahakimu na majaji, basi hakuna kosa kwake kwa sababu yeye ni mwakilishi tu.

Lakini, ikiwa uwakili unampeleka kumsaidia dhalimu, au kusaidia kumdhulumu mwingine, au kudanganya kwenye madai, au kutafuta mashahidi wa uongo, au vitendo vingine vya batili, basi ni haramu, na mwenye kufanya hivyo ni miongoni mwa wale wanaosaidia dhambi na uadui.

Na imethibiti kuwa alisema Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Msaidie ndugu yako akiwa ni dhalimu au mdhulumiwa." Wakasema: "Ewe Mtume tunamsaidiaje dhalimu?" Akasema: "Unamzuia asidhulumu" – yaani unapomzuia kutenda dhuluma, hiyo ndiyo kumsaidia.

Hivyo, kumsaidia dhalimu ni kumzuia na dhuluma. Lakini kama wakili anamsaidia dhalimu kufanikisha dhuluma, basi ni mshirika wake katika dhambi, na kazi yake ni munkar na anajitumbukiza katika adhabu ya Allah. Tunamwomba Allah atupe afueni.

Hali ni hiyo hiyo kwa kila mwakilishi, hata asipoitwa wakili. Ajue, kama anamsaidia mtu wake kufanya dhuluma na kuchukua haki za watu kwa batili, basi ni mshirika wake katika dhambi na ni dhalimu kama yeye.

Ninashauri kutojishughulisha na uwakili isipokuwa kwa mtu anayejua nafsi yake kuwa atafuata Sharia, atasaidia kuitekeleza, atamsaidia mdhulumiwa, na hatamsaidia dhalimu.

Lakini kama mtu ana tabia ya kupenda pesa kwa haki na bila haki, na kutetea mteji wake bila kujali haki au uongo, basi kwake haiwezi kuwa halali, bali lazima ajihadhari. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

صفر

DARASA LA WIKI

SEHEMU YA 1



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Hukumu na adabu za kumuosha maiti wa Kiislamu

## SEHEMU YA 2

**Katika toleo lililopita, tuliishia kwenye kipengele kilichozungumzia namna ya kuosha maiti kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu. Tulieleza mambo matatu yanayopendekezwa (Sunna) wakati wa kumuosha maiti wa Kiislamu.**
**Mambo hayo ni: kwanza, kuharakisha kumuosha; pili, kumuosha katika sehemu ya faragha iliyositirika; na tatu, kuhakikisha maji ya kutosha yanapatikana kwa ajili ya shughuli hiyo.**

Jambo la nne, inapendekezwa (ni Sunna) kuweka manukato yenye harufu nzuri mahali pa kuoshea maiti ili kuondoa au kuficha harufu inayoweza kutoka mwilini.

Tano, inapendekezwa kuweka majani ya mkunazi (sabuni) kwenye maji na kumuosha maiti mara mbili, kisha mara ya tatu kwa maji yaliyochanganywa na kafuri (manukato yenye harufu maalumu) au manukato mengine, ingawa kafuri ndiyo inayopendekezwa zaidi.

Sita, inapendekezwa maiti kuwekwa juu ya ubao au kitanda kilichoandaliwa kwa ajili hiyo, huku kichwa chake kikiwa juu kuliko sehemu nyingine za mwili ili kurahisisha maji kuteremka.

Saba, maiti avalishwe kanzu pana na kuoshwa akiwa ndani yake. Iwapo kanzu haipatikani au haiwezekani kumuosha akiwa ndani yake, sehemu iliyo kati ya kitovu na magoti ifunikwe kwa shuka au nguo yoyote.

Nane, hairuhusiwi kwa mwoshaji na wasaidizi wake kutazama sehemu za siri za maiti. Tisa, hairuhusiwi pia kugusa sehemu zake za siri. Kumi, inapendekezwa (ni Sunna) mwoshaji aandae vitambaa safi (au glove) kabla ya kuanza kumuosha.

Kumi na moja, jambo la kwanza baada ya kumweka maiti mahali pa kuoshea ni kumkalisha kwa upole bila kumnyoosha kikamilifu. Maiti aegemezwe nyuma kidogo, kisha mwoshaji apitishe mkono wake wa kushoto juu ya tumbo lake na kulibonyeza taratibu ili uchafu uliomo utoke.

Wakati huo, msaidizi amimine maji ili kuzuia harufu ya uchafu unaotoka mwilini isijitokeze.

Kumi na mbili, baada ya hapo maiti arudishwe katika hali ya kulala chali. Kisha mwoshaji, kwa kutumia mkono wake wa kushoto uliofungwa kitambaa (au glove), aoshe sehemu ya haja kubwa na sehemu zake za siri, kama anavyojisafisha mtu aliye hai baada ya kujisaidia.

Wanazuoni wamesema kiwango cha chini kabisa cha sanda ni nguo moja inayofunika mwili wote. Kinachopendekezwa kwa mwanaume ni nguo (pande) tatu nyeupe za pamba au katani. Ni haramu kwa mwanaume kutumia sanda ya hariri.

Kwa mwanamke, kinachopendekezwa (Sunna) ni nguo (pande) tano, na matumizi ya hariri si haramu kwake. Kuzidisha zaidi ya hapo ni ubadhirifu (matumizi mabaya), huku kutumia gharama kubwa kupita kiasi kukichukuliwa kuwa ni jambo la kuchukiza (makuruhu).

Kumi na tatu, akimaliza kuosha sehemu hizo mbili, amtawadhishe kama anavyotawadha mtu aliye hai, mara tatu.

Kumi na nne, akimaliza kumtawadhisha aoshe kichwa na ndevu zake kwa maji na sabuni. Pia inapendekezwa (ni Sunna) nywele za mwanamke zisukwe mafundo (misuko) matatu.

Kumi na tano, maiti alazwe ubavu wa kushoto na amiminiwe maji upande wa kulia wa mwili wake. Baada ya hapo, alazwe ubavu wa kulia na amiminiwe maji upande wa kushoto wa mwili wake. Huko ndiko kuosha mara moja, nako ndiko kuosha kwa lazima (wajibu).

Imepokewa kutoka kwa Imam Malik kwamba kinachozingatiwa si idadi ya kuosha, bali ni kupatikana kwa usafi. Mwoshaji anatakiwa kupitisha mkono tumboni mwa maiti kila mara anapoosha, lakini kwa upole zaidi kuliko mara iliyotangulia.

Kumi na sita, akimaliza kumuosha, amkaushe vizuri (amfute) ili kuzuia sanda kulowana na hivyo kupunguza uwezekano wa mwili kuharibika haraka.

### Namna ya kumkafini (kumvisha sanda)

Ama kuhusu namna ya kumkafini (kumvisha sanda) maiti, wanazuoni wamesema: Mosi, itandazwe sanda iliyo bora na pana zaidi, kisha inyunyiziwe manukato. Juu yake itandazwe nguo ya pili, nayo inyunyiziwe manukato. Halafu itandazwe nguo ya tatu, ambayo pia inyunyiziwe manukato. Baada ya hapo, maiti awekwe juu ya sanda hizo akiwa amelala chali.

Pili, kichukuliwe kiasi cha pamba, kiwekwe manukato, kisha kiwekwe katikati ya makalio yake hadi kufikia sehemu ya haja kubwa ili kuzuia chochote kinachoweza kutoka wakati maiti anaposogezwa.

Tatu, kichukuliwe kiasi cha pamba, kiwekwe manukato, kisha kiwekwe kwenye matundu ya mwili, kama vile puani, masikioni na kwenye majeraha yaliyo wazi, ikiwa yapo.

Nne, manukato yanyunyiziwe kwenye viungo vya kusujudia, navyo ni paji la uso, pua, viganja vya mikono kwa ndani, magoti na nyayo za miguu, kwa ajili ya kuviheshimu.

Tano, kisha maiti afungwe kwa nguo ya kwanza ya sanda iliyo karibu na mwili wake. Nguo hiyo ikunjwe juu yake; upande mmoja ukunjwe juu ya ubavu wake wa kulia, kisha upande mwingine ukunjwe juu ya ubavu wake wa kushoto. Baada ya hapo ifungwe nguo ya pili, kisha nguo ya tatu.

Sita, baada ya sanda kufungwa, sehemu iliyobaki upande wa kichwa ikusanywe na kurudishwa juu ya uso na kifua chake kadiri inavyotosha. Sehemu iliyobaki upande wa miguu iwekwe juu ya nyayo na miguu yake.

Saba, sanda ifungwe kwa kamba ili kuzuia isifunguke wakati wa kubebwa. Maiti anapowekwa kaburini, kamba hizo zifunguliwe. Baada ya hapo, maiti anyunyiziwe kiasi cha manukato.

صفر

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Teknolojia ya AI: Neema ya dunia, mtihani wa Akhera

Hakuna shaka kuwa teknolojia ya Akili Unde (AI) imefungua milango mipya ya maendeleo katika nyanja mbalimbali za maisha. Katika sekta ya afya, AI inasaidia wataalamu kuchanganua taarifa kwa ufanisi na kuboresha huduma kwa wagonjwa.

Katika elimu, AI imewasaidia wanafunzi kupata maarifa kwa urahisi zaidi na kuongeza uwezo wao wa kujifunza. Aidha, katika biashara imekuwa chombo muhimu kinachowawezesha wafanyabiashara kuelewa mahitaji ya wateja, kuboresha huduma na kuongeza ufanisi wa shughuli zao.

Kwa vijana, AI imefungua fursa za taaluma mpya, zikiwamo uhandisi wa Akili Unde, uchambuzi wa data, usalama wa mitandao na ubunifu wa kidijitali.

Katika nchi zinazoendelea, matumizi ya AI yanaweza kuwa chachu ya kuharakisha maendeleo katika sekta za kilimo, afya na elimu, iwapo yataongozwa na mipango madhubuti na matumizi sahihi. Allah anasema: “Na tafuta katika yale aliyokupa Mwenyezi Mungu makazi ya Akhera, na wala usisahau sehemu yako ya dunia.” [Qur’an, 28:77].

Aya hii inaonesha uwiano kati ya maendeleo ya dunia na maandalizi ya Akhera. Mwanadamu ameruhusiwa kutumia neema za dunia kwa manufaa yake, lakini hapaswi kusahau wajibu wake kwa Muumba wake.

## AI na changamoto ya maadili

Pamoja na kuleta manufaa makubwa, teknolojia ya Akili Unde imeibua changamoto zinazohitaji umakini wa hali ya juu. Matumizi yake yanaweza kuwa ya manufaa au ya madhara, kutegemeana na nia na maadili ya mtumiaji.

Miongoni mwa changamoto kubwa zinazotokana na AI ni kusambaza taarifa za uongo, kutengeneza picha na video bandia, kuvamia faragha za watu na kufanya udanganyifu.

Katika Uislamu, ukweli ni miongoni mwa misingi muhimu ya maisha ya Muumini. Allah anasema: “Enyi mliyoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli.” [Qur’an, 9:119]. Katika zama ambazo taarifa zinaweza kubuniwa na kusambazwa ndani ya sekunde chache, mafunzo haya yana umuhimu mkubwa zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

Namna mtu anavyotumia maarifa yake na teknolojia aliyonayo ni sehemu ya uwajibikaji wake katika jamii. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Inatosha mtu kuwa muongo kwa kusimulia kila analolisikia.” [Sahih Muslim].

Hivyo yatupasa kuwa waangalifu na kujiepusha na kusambaza habari bila kuzihakiki.

## Matumizi ya teknolojia na hesabu ya Akhera

Mojawapo ya misingi mikuu ya imani ya Kiislamu ni kwamba mwanadamu atawajibika kwa matendo yake yote mbele ya Allah Ta’ala. Allah anasema: “Basi yule atakayefanya kheri yenye uzito wa chembe (mfano wa atomu) ataiona. Na yule atakayefanya shari yenye uzito wa chembe (kama atomu) ataiona.” [Qur’an 99:7–8].

Kwa mantiki hiyo, matumizi ya teknolojia nayo yatakuwa sehemu ya matendo ya mwanadamu yatakayohesabiwa Siku ya Kiyama. Teknolojia ni nyenzo yenye uwezo wa kuleta manufaa au madhara, kutegemea namna inavyotumiwa.

Mtu anayetumia AI kueneza maarifa yenye manufaa, kusaidia matibabu ya wagonjwa, kuwahudumia wenye uhitaji au kuchochea maendeleo katika jamii, anatumia neema hiyo kwa njia yenye tija na inayoweza kumpatia thawabu.

Ama yule anayetumia kwa madhumuni ya kudanganya watu, kueneza chuki au kusababisha madhara kwa wengine, anapaswa kutambua kuwa uwezo huo ni amana yenye dhima kubwa mbele ya Allah. Matumi zi mabaya ya teknolojia yaweza kuwa miongoni mwa matendo ambayo mwanadamu atawajibishwa kwayo Siku ya Kiyama.

## Jukumu la vijana katika kuongoza teknolojia

Kizazi kipya ndicho kitakachobeba jukumu kubwa la kuamua mwelekeo wa Akili Unde (AI) katika miaka ijayo. Changamoto iliyopo si kuikataa teknolojia, bali kuhakikisha kwamba inatumika kwa busara, maadili na hekima kwa manufaa ya jamii.

Historia ya Uislamu inaonesha kuwa Waislamu walitoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sayansi na ustaarabu wa dunia.

Wanazuoni kama Al–Khwarizmi katika taaluma ya hisabati na Ibn Sina katika fani ya tiba walitumia maarifa yao kwa lengo la kuwanufaisha wanadamu.

Vijana wa sasa wana nafasi kubwa ya kuendeleza urithi huo kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuibua ubunifu unaoweza kuchangia maendeleo ya jamii.

Wanapaswa kuwa wabunifu wanaotengeneza suluhisho kwa changamoto mbalimbali, badala ya kuwa watumiaji wanaotegemea teknolojia bila kuichambua, kuielewa au kuitumia kwa ubunifu.

## AI isitufanye tusahau ibada

Licha ya maendeleo makubwa ya teknolojia na kuongezeka kwa matumizi ya AI, mwanadamu bado ana wajibu wa kumtambua na kumuabudu Muumba wake.

Maendeleo ya sayansi na teknolojia hayaondoi jukumu hilo, bali yanapaswa kutumiwa kwa namna inayomtukuza Muumba na kuwanufaisha wanadamu. Allah anasema: “Na Sikuwaumba majini na wanadamu ila waniabudu Mimi.” [Qur’an, 51:56].

Ingawa AI inaweza kuwa nyenzo muhimu ya kumsaidia mwanadamu katika nyanja mbalimbali za maisha, haiwezi kuchukua nafasi ya mwongozo wa moyo, huruma ya kibinadamu au uhusiano wa kiroho kati ya mwanadamu na Muumba wake.

Ujumbe muhimu kwa kizazi cha sasa ni mmoja: Tumia teknolojia kama nyenzo ya kujenga dunia na kuboresha maisha ya wanadamu, lakini usisahau kujiandaa na Akhera.

صفر

MAKALA MAALUM

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

# Si kila mlango uliofungwa ni hasara; huenda ni rehema ya Allah

Wakati mwingine tunatumia muda mwingi kuomboleza mlango uliofungwa kiasi cha kusahau kwamba Allah ndiye aliyeufunga. Tunahuzunika kwa kazi tuliyoikosa, ndoa iliyochelewa, biashara iliyoshindikana, nafasi ya masomo iliyopita au uhusiano uliovunjika. Kwa macho yetu, hayo yanaonekana kuwa hasara. Lakini kwa mtazamo wa tawakkul, huenda baadhi yake ni rehema kubwa ya Allah iliyojificha katika sura ya kukataliwa.

Mwanadamu huona sehemu ndogo tu ya safari yake. Anaweza kuona uzuri wa fursa, lakini asione hatari iliyojificha ndani yake. Anaweza kutamani jambo fulani kwa sababu linaonekana kufaa leo, bila kujua litampeleka wapi kesho. Allah, kwa upande mwingine, anajua mwanzo, mwisho na yote yaliyo katikati.

Hii ndiyo sababu kuamini mpango wa Allah hakumaanishi kuelewa kila jambo linalotokea. Ni kukubali kwamba hekima Yake inafika mahali ambapo macho na akili zetu haziwezi kufika. Qur'an inatukumbusha kuwa tunaweza kuchukia jambo ambalo lina kheri kwetu, au kupenda jambo ambalo lina shari kwetu; Allah anajua, nasi hatujui [Qur'an, 2:216].

Hata hivyo, tawakkul haimaanishi kukaa bila kufanya juhudi. Muislamu anawajibika kuchukua sababu: kusoma kwa bidii, kutafuta kazi, kupanga biashara, kuweka akiba, kutafuta matibabu, kushauriana na watu wenye ujuzi na kuomba dua. Tunawajibika kwa juhudi zetu, lakini hatumiliki matokeo.

Mkulima analima, anapanda na kupalilia, lakini hawezi kuamuru mvua inyeshe. Mwanafunzi anasoma, anafanya mazoezi na kuingia katika mtihani, lakini hawezi kudhibiti kila kitakachojitokeza. Mtu anaweza kujiandaa vizuri kwa usaili wa kazi, lakini uamuzi wa mwisho ukawa tofauti na matarajio yake. Katika mazingira hayo, wajibu wa mtu ni kufanya sehemu yake kwa uaminifu na kumwachia Allah yaliyobaki.

Tawakkul inaleta mabadiliko muhimu ya kisaikolojia. Badala ya kuuliza, "Nitadhibitije kila kitu?" mtu huanza kujiuliza, "Je, nimefanya nililoweza, na je, nimemkabidhi Allah nisiloweza?"

Swali la kwanza huzaa wasiwasi kwa sababu linataka mwanadamu abebe uwezo ambao hana. Swali la pili huunganisha uwajibikaji na utulivu. Linamzuia mtu kutumia dini kama kisingizio cha uzembe, lakini pia linamwondolea mzigo wa kujilaumu kwa matokeo yaliyokuwa nje ya uwezo wake.

Tawakkul haifuti maumivu wala haikatazi machozi. Badala yake, huupa moyo msingi wa kusimama katikati ya maumivu. Hali inaweza kubaki ileile, jibu likachelewa na kesho ikaendelea kutokuwa na uhakika. Lakini moyo hubadilika: hauoni tena kila kilichopotea kama mwisho wa safari.

Pengine kazi uliyoikosa ingekuweka katika mazingira mabaya. Huenda ndoa iliyochelewa inakuepusha na uamuzi wa haraka. Inawezekana biashara iliyoshindikana imekufundisha nidhamu itakayookoa mradi mkubwa zaidi baadaye. Haya ni mambo yanayowezekana, si maelezo tunayoweza kuyathibitisha kuhusu kila tukio. Hatupaswi kudai tunaijua sababu maalumu ya Allah. Tunachoweza kuamini ni kwamba ujuzi Wake ni mpana kuliko wetu.

Hivyo, mlango unapofungwa, usiache kujaribu. Chunguza makosa yako, jifunze, omba ushauri na utafute mlango mwingine. Lakini usifikiri thamani ya maisha yako imefungwa pamoja na fursa hiyo. Wakati mwingine kukataliwa ni ulinzi, kuchelewa ni maandalizi na kupoteza ni kuelekezwa kwingine.

Qur'an inasema: "Na anayemtegemea Allah, basi Yeye humtosha" [Qur'an, 65:3]. Tawakkul haitupi mamlaka ya kuamua matokeo. Inatupa nguvu ya kufanya wajibu wetu bila kuwa watumwa wa matokeo. Si kila mlango uliofungwa ni hasara; mingine ni rehema ya Allah inayotuelekeza kwenye mlango unaotufaa zaidi.

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383



# Watoto wadogo hujifunza kwa kuiga, onesha mfano

Mtoto mmoja alisikika akimtukana mwenzake kwa maneno makali. Mama yake alishtuka na kumkaripia: "Umejifunza wapi matusi hayo?" Mtoto hakujibu, lakini ukweli ulikuwa wazi. Siku chache kabla, alikuwa amemsikia mzazi huyo akitumia maneno yaleyale alipokuwa amekasirika.

Jioni nyingine, mzazi akamwambia mtoto: "Zima michezo, nenda kasome." Mtoto akachukua kitabu, akakaa nacho kwa muda mfupi, kisha akarudi kucheza. Wakati huo, mzazi alikuwa sebuleni akitazama tamthilia kwenye televisheni na kuperuzi mitandaoni kupitia simu janja.

Wakati mtoto anapewa amri ya kusoma, mazingira yote ya nyumbani yalikuwa yakimfundisha kufanya jambo tofauti. Hapo ndipo wazazi wengi hukosea. Hawawi mfano kwa watoto wao badala yake wanategemea watoto watii maelekezo.

Wanataka watoto wasome, lakini hawaoni kitabu mikononi mwa mzazi. Wanataka wazungumze kwa heshima, lakini husikia watu wazima wakitukana. Wanataka wawe na nidhamu ya matumizi ya simu, lakini kila mazungumzo ya kifamilia yanakatizwa na skrini.

Watoto hujifunza kwa kusikiliza, lakini hujifunza zaidi kwa kutazama. Katika saikolojia ya elimu, hii huitwa ujifunzaji kwa uchunguzi: mtoto humwangalia mtu anayemwamini, hufuatilia tabia yake na kujaribu kuiga. Kwa hiyo, mzazi ni mwalimu hata wakati hajafungua kitabu wala kutoa mawaidha.

Nadharia hii inaweza kutusaidia kueleza tabia ya walimu wa chekechea kuwa kama watoto.

## Kusoma ni ujuzi, si amri

Kauli ya "nenda kasome" haitoshi. Mtoto anaweza kukaa mbele ya kitabu kwa saa mbili bila kuelewa anachofanya. Huenda hajui aanzie wapi, asome kwa muda gani, aandike nini au apumzike lini.

Mzazi anapaswa kumfundisha namna ya kusoma. Anza kwa kugawa kazi kubwa katika sehemu ndogo. Badala ya kusema, "Maliza somo lote," sema: "Tusome kurasa hizi mbili, kisha unieleze ulichoelewa." Msaidie kutengeneza ratiba yenye muda wa kusoma, kupumzika na kucheza. Usimpime kwa muda aliokaa na kitabu pekee; angalia kama ameelewa, ameandika au ameweza kueleza jambo alilosoma.

Mtoto pia anahitaji mahali pa kujifunzia penye utulivu. Televisheni inapokuwa imefunguliwa, simu zikipiga kila dakika na watu wakizungumza kwa sauti, ni vigumu kutarajia umakini wa hali ya juu.

## Zima televisheni, chukua kitabu

Mbinu inaweza kuwa ndogo sana. Fika muda wa kusoma, zima televisheni. Weka simu pembeni. Chukua kitabu, gazeti au makala, kisha kaa karibu na mtoto. Mwambie: "Huu ni muda wetu wa kusoma. Wewe soma chako, nami nitasoma changu."

Mara ya kwanza mtoto anaweza kushangaa. Baada ya siku kadhaa, atasoma bila kuhisi kuwa anaadhibiwa. Ataanza kuona usomaji kama sehemu ya maisha ya familia, si kazi ya watoto pekee.

Mnaweza pia kusoma pamoja. Mtoto asome aya moja kwa sauti, mzazi asome inayofuata. Muulize maswali mepesi: "Umeelewa nini?" "Ni neno gani jipya?" "Unadhani kwa nini mhusika alifanya hivyo?" Mazungumzo hayo humfundisha kufikiri, si kukariri tu.

## Tengeneza utamaduni, si vitisho

Nidhamu hukua vizuri ndani ya utamaduni kuliko ndani ya amri. Nyumba yenye vitabu, mazungumzo ya kielimu na mipaka ya matumizi ya skrini humrahisishia mtoto kujenga tabia ya kusoma.

Pongeza juhudi, si alama pekee. Mtoto akikaa na kujaribu, sema: "Nimeona umejitahidi." Akishindwa, msaidie kugundua alikosea wapi. Vitisho, kulinganisha watoto na kuwadhihaki vinaweza kumfanya mtoto aogope masomo badala ya kuyapenda.

Mfano huo unapaswa kuonekana katika tabia nyingine pia. Unapotaka mtoto aseme "tafadhali," "asante" na "samahani," anapaswa kusikia maneno hayo yakitumika kwake. Ukimkosea, mwombe msamaha. Ukikasirika, onyesha namna ya kutulia bila matusi.

Malezi bora hayaanzi kwa kuuliza, "Kwa nini mtoto wangu hanisikilizi?" Wakati mwingine huanza kwa kuuliza: "Ni jambo gani ananiona nikifanya kila siku?"

صفر

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR

0773 181 494

SEHEMU YA 18



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Katika kipindi hiki ndipo Mtume Musa (amani ya Allah imshukie) alipopewa kitabu chenye hukumu, sharia na miongozo kwa wana wa Israil, baada ya kutakiwa afanye ibada kwa wingi masiku kadhaa kama inavyoeleza Qur'an Takatifu: "Na tulimuahidi Musa siku 30 (afanye ibada mfululizo kisha tumpe Kitabu), na tukazitimiza kwa 10 ikatimia miadi ya Mola wake (ya kumpa hiyo Taurati) siku 40. Na Musa akamwambia ndugu yake Haruni, 'Shika nafasi yangu (katika kuwaongoza) watu wangu, na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu'" [Qur'an, 7:143].**

### Musa amuomba Mola wake ajioneshe amuone

Kwa hiyo Musa akawa mbali na watu wake masiku kadhaa. Alipofika mlimani, Mola wake akamsogeza na kumesemesha. Shauku ya kutaka kumuona ilimjia, kama inavyoeleza Qur'an:

"Na alipofika Musa katika miadi yetu akasema, 'Ewe Mola wangu nioneshe (nafasi yako) ili nikuone.' Akasema, 'Hutoniona lakini tazama jabali (mbele yako) kama litabaki mahala pake (bila ya kupasuka) basi utaniona.' Basi Mola wake alipojionesha (alipojidhihirisha) kwenye mlima aliufanya wenye kuvunjika-vunjika na Musa akaanguka hali ya kuzimia. Alipozindukana alisema, 'Umetakasika (Wewe ndiye Mtukufu), natubu Kwako na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini (kwamba huonekani)'" [Qur'an, 7:144].

"Allah akamwambia, 'Ewe Musa, Mimi nimekuchagua juu ya watu wote kwa ujumbe wangu na kwa kusema nawe (nyuma ya pazia), basi pokea haya niliyokupa (tu) na uwe miononi mwa wanaoshukuru'" [Qur'an, 7:145].

Kisha Mtume Musa akapokea Mbao (Kitabu) kilichojaa kila walilolihitaji wana wa Israil: mawaidha na uchanganuzi wa sharia na hukumu, na kutakiwa azishike na awaamrishe watu wake wazishike kisawasawa, na pia aliambiwa kwamba Allah atawaonesha nyumba (mwisho) wa wavunjao amri zake.

### Musa apewa habari ya kupotoka kwa watu wake

Mtume Musa akiwa bado kwenye miqati (kwenye mlima aliosemezwa), Allah akamuuliza: "Na ni kitu gani kimekutia haraka ukawaacha watu wako ewe Musa?" Akasema: "Hao wako nyuma wananifuata, na nimefanya haraka kukujia Mola wangu ili uzidi kuniridhia." Akasema: "Basi sisi tumewatia mtihani watu wako baada yako na wamepotezwa na Samiri." [Qur'an, 20:83-85].

### Musa arudi kwa watu wake

"Musa akarejea kwa watu wake kwa hasira na kusikitika, akasema: "Enyi watu wangu, je Mola wenu hakukuahidini ahadi njema? Je umekuwa mrefu kwenu muda wa ahadi hiyo (mnaona haitotimizwa) au mumetaka zikushukieni hasira za Mola wenu, na kwa hivyo mmevunja ahadi yangu?" [Qur'an, 20:86].

"Wakasema, 'Sisi hatukuvunja ahadi yake kwa hiari yetu, lakini tulibebeshwa mizigo ya watu (vyombo vya dhahabu tulivyoviazima kwa wanawake wa Misri), tukaitupa motoni (ikayeyuka na kuundwa mungu).' Na hivyo ndivyo alivyotoa shauri Samiri. Akawatolea (akawatengenezea) watu ndama kiwiliwili kinachotoa sauti na akasema, 'Huyu ndiye mungu wenu na mungu wa Musa lakini (Musa) amesahau, (amekwenda kumtafuta majangwani).'" [Qur'an, 20:88].

(Musa aliporejea) akasema: "Ewe Haruni, nini kilichokuzuia (usinifuate) ulipowaona wamepotea, hukunifuata! au (na wewe) umeasi amri yangu?! (alisema hayo huku akimshika na kumtikisa)

Akasema Haruni: "Ewe mwana wa mama yangu, usinishike ndevu zangu wala kichwa changu, kwa hakika niliogopa (kuondoka na baadhi nikawaacha wengine) usije ukasema, 'Umewafarikisha (umewagawa) wana wa Israil na hukungojea kauli yangu'"[Qur'an, 20:92-93].

Katika mahala pengine inelezwa: "Na Musa aliporudi kwa watu wake huku akiwa amekasirika na kuhuzunika alisema, 'Unaibu mbaya mmenifanyia nyuma yangu baada ya kuondoka! Je mumeitangulizia amri ya Mola wenu (mukafanya yenu kabla ya kujua anayokuamrisheni)!?'

Na akazitupa mbao (kwa hasira) na akakikamata kichwa cha ndugu yake kukivuta kwake (kama anataka kumpiga kwa hasira). Akasema Haruni, 'Ewe (ndugu yangu) mwana wa mama yangu, hakika watu hawa wamenidharau (hawakunisikiliza) na wakakaribia kuniua, basi usiwafurahishe maadui juu yangu wala usiniweke pamoja na watu (waovu) madhalimu'" [Qur'an, 7:150].

Kitendo hiki kilichofanywa na wana wa Israil kiliwatiwa katika hatia, lawama na hasira kubwa kutoka kwa Mola wao kama inavyoelezwa katika Qur'an: "Je hawakuona kuwa (ndama huyo) hawarudishii neno wala hawamilikii dhara wala manufaa?"

### Mtume Haruni kuwakataza

Haruni aliwakataza watu wake kuabudu ndama lakini hawakumsikiliza. "Na Haruni aliwaambia zamani, 'Enyi watu wangu, hakika nyinyi mumejaribiwa tu na kwa yakini Mola wenu ni yule Mungu mwenye kurehemu basi nifuateni na tiini amri yangu (acheni kumuabudu huyo ndama).' Wakasema, 'Hatutoacha kabisa kumuabudu mpaka Musa arejee kwetu.' [Qur'an, 20:90-91].

*Itaendelea inshaAllah*

صَفَر

# Kujiamini kwa kiongozi kunaonekana katika mambo haya 7

**Watu wengi hudhani kujiamini ni kuzungumza kwa sauti kubwa, kutokuwa na mashaka au kuwa na majibu ya kila swali. Lakini kujiamini kwa kweli si kujiona bora kuliko wengine. Ni uwezo wa kuchukua hatua, kukubali udhaifu, kusimamia hisia na kuendelea kujifunza bila kupoteza thamani yako. Kujiamini hakupimwi kwa namna kiongozi anavyojitokeza wakati mambo ni mepesi bali anapokabiliwa na uamuzi mgumu, anapokosolewa au anapolazimika kukiri kuwa hajui. Zifuatazo ni aina saba za kujiamini zinazoweza kukujenga.**

## *Mosi,* kujiamini katika kufanya uamuzi

Kiongozi hawezi kusubiri mpaka kila jambo liwe wazi kwa asilimia 100. Wakati mwingine taarifa huwa chache, muda huwa mfupi na athari za uamuzi huwa kubwa. Kujiamini katika maamuzi ni uwezo wa kuchanganua taarifa zilizopo, kusikiliza ushauri na kuchagua njia bila kukimbia wajibu.

Haimaanishi kufanya maamuzi kwa pupa. Kiongozi mwenye busara hutofautisha ujasiri na uzembe. Akigundua kuwa uamuzi wake haukuwa sahihi, hubadili mwelekeo badala ya kuulinda kwa sababu tu ulitolewa naye.

## *Pili,* kujiamini katika kupokea mrejesho

Kukosolewa huumiza, hasa tunapoamini tumefanya vizuri. Mtu asiyejiamini anaweza kujitetea, kutoa visingizio au kumshambulia anayemkosoa. Kiongozi anayejiamini husikiliza hata ukweli mgumu bila kuona kila ukosoaji kama shambulio.

Hata hivyo, si kila mrejesho ni sahihi. Kujiamini kunamwezesha mtu kuuliza: Kuna ukweli gani hapa? Niboreshe nini? Nini hakina ushahidi? Lengo si kukubali kila kauli, bali kuitumia kama kioo cha kujichunguza.

## *Tatu,* kujiamini katika kukubali udhaifu

Maneno "sijui," "nimekosea" na "nahitaji msaada" yanaweza kuonekana kama ishara ya udhaifu. Kwa hakika, kuyasema huhitaji nguvu ya ndani. Kukubali usichokijua kunafungua nafasi ya kujifunza na kuwapa wenye maarifa nafasi ya kuchangia.

Kiongozi anayejifanya kujua kila kitu huwafundisha wengine kuficha mapungufu yao. Anayekubali udhaifu hujenga mazingira ambayo watu wanaweza kuuliza na kurekebisha makosa kabla hayajaleta madhara makubwa.

## *Nne,* kujiamini katika kukabidhi majukumu

Baadhi ya viongozi hushindwa kuwaamini wengine kwa sababu wanaamini hakuna anayeweza kufanya kazi vizuri kama wao. Matokeo yake ni kuchoka, kuchelewesha maamuzi na kuwanyima wengine nafasi ya kukua.

Kukabidhi jukumu si kulikimbia. Ni kuchagua mtu anayefaa, kueleza matokeo yanayotarajiwa, kumpa rasilimali na kufuatilia bila kuingilia kila hatua. Kiongozi mwenye kujiamini hafurahii kuwa mtu pekee muhimu; hujenga timu inayoweza kufanya kazi hata asipokuwapo.

## *Tano,* kujiamini kihisia

Hasira, hofu, huzuni na wasiwasi ni sehemu ya maisha. Kujiamini kihisia si kutokuwa na hisia, bali ni kuzitambua bila kuziacha ziamue kila jambo. Kiongozi anaweza kukasirika, lakini akaamua kutotoa jibu mpaka atulie.

Mtu anayekandamiza hisia zote anaweza kuonekana imara, lakini hisia hizo hujitokeza kwa namna nyingine—kama ukali, ukimya au maamuzi ya kulipiza kisasi. Ukomavu ni kuhisi kikamilifu na bado kuchagua jibu lenye kusudi.

## *Sita,* kujiamini katika kuweka mipaka

Kusema "hapana" ni jambo gumu kwa watu wanaotaka kukubalika na kila mtu. Lakini anayekubali kila ombi huweza kupoteza muda, afya na vipaumbele vyake.

Mipaka inalinda mambo yenye thamani. Kiongozi anaweza kukataa ombi kwa heshima, kueleza sababu na, ikiwezekana, kupendekeza njia nyingine. Si kila anayekasirishwa na mpaka wako ana maana kuwa mpaka huo si sahihi.

## *Saba,* kujiamini kwa unyenyekevu

Hii ndiyo nguzo inayounganisha nyingine zote. Ni kuwa na msimamo bila kiburi, kuwa na uwezo bila kuwadharau wengine na kuongoza bila kujifanya mkamilifu. Mtu huyu anaamini kile anachoweza kufanya, lakini anaendelea kuwa mdadisi na tayari kujifunza.

Kujiamini kwa afya hakupigi kelele kutafuta sifa. Huonekana katika uwajibikaji, utulivu na namna tunavyowatendea wengine. Mwishowe, kiongozi bora si mwenye majibu yote, bali anayethubutu kuamua, kusikiliza, kukiri mapungufu na kukua pamoja na anaowaongoza.

Na Junaynat Ally Dama

# Njia bora ya kujifunza akili unde ni kuitumia

**Watu wengi wanataka kujifunza akili unde kwa kusoma vitabu, kujiunga na kozi, kusikiliza vipindi vya sauti au kufuatilia mijadala ya wataalamu. Njia hizo zina umuhimu wake. Zinasaidia kuelewa dhana, istilahi na mwelekeo wa teknolojia. Hata hivyo, maarifa ya kweli ya kutumia akili unde hayapatikani kwa kusoma pekee. Njia ya haraka zaidi ni kuanza kufanya kazi halisi nayo: kuijaribu, kuikosea, kuiboresha na kupima matokeo yake.**

**Akili unde ni kama chombo kingine cha kazi. Mtu hawezi kuwa dereva mzuri kwa kusoma sheria za barabarani pekee. Ni lazima aingie barabarani, ajifunze kushika usukani, kutathmini mazingira na kurekebisha makosa. Vivyo hivyo, ujuzi wa akili unde hujengwa kwa matumizi ya mara kwa mara katika kazi za kila siku.**

## Chagua kazi moja unayoifanya mara kwa mara

Hatua ya kwanza ni kuchagua kazi halisi unayoifanya kila wiki. Inaweza kuwa kuandika barua, kufupisha kumbukumbu za vikao, kuandaa ripoti, kufanya utafiti wa hadhira, kutengeneza mawazo ya matangazo, kupanga maudhui ya mitandao ya kijamii au kuandaa maswali ya mahojiano.

Usianze na kazi ngumu sana. Chagua kazi inayojirudia na inayotumia muda mwingi. Lengo si kuonyesha kwamba unaweza kutumia teknolojia ya kisasa, bali kutatua tatizo linalokukabili.

## Andika hatua zote za kazi hiyo

Kabla ya kutumia akili unde, fanya kazi hiyo kwa njia ya kawaida na uandike kila hatua unayopitia. Bainisha taarifa unazokusanya, maamuzi unayofanya na muda unaotumia.


Hatua hii inaweza kuonekana ya kuchosha, lakini husaidia kutambua sehemu ambazo akili unde inaweza kusaidia. Bila kuelewa mchakato wa kawaida, ni rahisi kutumia AI katika sehemu isiyohitaji msaada na kupuuza sehemu inayopoteza muda zaidi.

## Itumie kama msaidizi wa kazi

Baada ya kuelewa mchakato, anza kutumia akili unde kama msaidizi. Tengeneza maelekezo tofauti kwa kila hatua. Jaribu aina kadhaa za maelekezo, linganisha majibu na hifadhi yale yanayotoa matokeo bora.

Kwa mfano, badala ya kuiambia tu "niandikie ripoti," eleza aina ya ripoti, hadhira, urefu, mtindo na taarifa zinazopaswa kuingizwa. Kadiri maelekezo yanavyokuwa wazi, ndivyo uwezekano wa kupata matokeo yanayofaa unavyoongezeka.

Majaribio hayatafanikiwa kila wakati. Baadhi ya majibu yatakuwa dhaifu, marefu au yasiyo sahihi. Lakini makosa hayo ndiyo sehemu muhimu ya kujifunza. Yanakuonyesha mipaka ya mfumo na namna ya kuboresha maelekezo yako.




## Rahisisha kazi zinazochosha

Baada ya kupata njia inayofanya kazi, tafuta namna ya kupunguza hatua zinazojirudia. Unaweza kuunganisha akili unde na lahajedwali, barua pepe, kalenda au mifumo ya kuhifadhi taarifa.

Hata hivyo, si lazima uanze na mfumo mgumu. Lengo ni kuondoa hatua ndogo zinazopoteza muda. Kama kazi ya dakika 30 inaweza kufanyika kwa dakika 10 bila kupunguza ubora, tayari kuna manufaa.

## Hakiki matokeo yote

Kila jibu la akili unde linapaswa kukaguliwa. Chunguza kama kuna taarifa za kubuni, makosa ya lugha, sauti isiyofaa au maudhui yanayoweza kukiuka faragha.

Akili unde inaweza kutoa majibu yenye kuonekana ya kitaalamu huku yakiwa na makosa. Kwa hiyo, mtumiaji ndiye anayebaki na wajibu wa mwisho. Ondoa taarifa nyeti na usiingize siri za watu au taasisi katika mifumo usiyoifahamu vizuri.

Pima kama matumizi yana faida

Pima mambo mawili rahisi: Je, kazi imefanyika kwa haraka zaidi? Je, ubora wa matokeo umeongezeka?

Kama akili unde haijaokoa muda wala kuboresha kazi, huenda haikufaa katika mchakato huo. Si kila kazi inapaswa kuendeshwa kwa AI. Wakati mwingine njia ya kawaida huwa bora zaidi.

## Shiriki ulichojifunza


Kushirikisha wengine majaribio yako kunakusaidia kuelewa zaidi. Eleza kilichofanikiwa, kilichoshindikana na marekebisho uliyofanya. Hii inaweza kufanyika katika kikao cha ofisi, darasani, kwenye makala au mtandao wa kitaaluma.

Ujuzi wa akili unde haujengwi kwa kutafuta maelekezo kamili tangu mwanzo. Unajengwa kwa kuchagua kazi halisi, kujaribu, kuhakiki, kupima na kurudia. Ukifanya hivyo katika kazi tatu tofauti ndani ya mwezi mmoja, utakuwa umejifunza zaidi kuliko mtu aliyesoma maelezo mengi bila kufanya jaribio hata moja.

صفر

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



# Viungo vyako vinahitaji nini ili viendelee kuwa na afya?

Mwili wa binadamu ni mfumo wa viungo vinavyotegemeana. Moyo husambaza damu, mapafu huingiza oksijeni, figo huchuja uchafu na ubongo huratibu shughuli nyingi. Kiungo kimoja kinapoathirika, vingine vinaweza kubeba mzigo wa ziada.


Mitandao ya kijamii hupenda kutoa ushauri mfupi, kama "tembea kwa ajili ya moyo" au "kunywa maji kwa ajili ya figo." Ushauri huo unaweza kuwa mwanzo mzuri, lakini afya ya kiungo haitokani na tabia moja pekee. Inahitaji mchanganyiko wa lishe bora, mazoezi, usingizi, maji, uchunguzi wa afya na kuepuka vitu hatarishi.

## Moyo unahitaji mwili unaosogea

Kutembea mara kwa mara husaidia kuimarisha moyo, kuboresha mzunguko wa damu na kudhibiti shinikizo la damu. Pia huchangia udhibiti wa sukari na lehemu katika damu.

Shirika la Afya Duniani linashauri watu wazima kufanya angalau dakika 150 hadi 300 za mazoezi ya wastani kwa wiki. Kutembea kwa mwendo wa haraka, kuendesha baiskeli na kufanya shughuli za nyumbani ni sehemu ya mazoezi hayo.

Mazoezi peke yake hayatoshi. Moyo unahitaji pia chakula chenye afya, uzito unaofaa, usingizi wa kutosha na kuepuka tumbaku. Shinikizo la damu, sukari na lehemu vinapaswa kupimwa kwa vipindi vinavyoshauriwa na mtaalamu.



## Ubongo na saa ya mwili vinahitaji usingizi

Usingizi huupa ubongo nafasi ya kupanga kumbukumbu, kuimarisha umakini na kuratibu hisia. Ratiba inayobadilika kila siku inaweza kuvuruga saa ya mwili—mfumo wa ndani unaodhibiti nyakati za kulala na kuamka.

Weka muda unaokaribiana wa kulala na kuamka kila siku. Punguza matumizi ya simu muda mfupi kabla ya kulala, epuka vinywaji vyenye kafeini usiku na tengeneza mazingira tulivu ya kulala.

Kujifunza stadi mpya pia huuchochea ubongo na mfumo wa neva. Kusoma, kuandika, kujifunza lugha, kushona au kutumia teknolojia mpya huupa ubongo changamoto yenye manufaa. Hata hivyo, madai kwamba kujifunza pekee "huimarisha mfumo wa neva" yanarahisisha mno suala pana la afya.

## Mifupa inahitaji lishe, mazoezi na vitamini D

Mwanga wa jua husaidia ngozi kutengeneza vitamini D, inayohitajika katika matumizi ya madini ya kalsiamu na afya ya mifupa. Hata hivyo, jua kali linaweza kuharibu ngozi. Muda salama wa kupata mwanga hutegemea mazingira, hali ya hewa na ngozi ya mtu.

Mifupa inahitaji pia vyakula vyenye kalsiamu na protini. Mazoezi yanayobeba uzito wa mwili, kama kutembea na kupanda ngazi, husaidia kuitunza.

## Mapafu yanahitaji hewa safi

Kupumua kwa kina na taratibu kunaweza kusaidia kupunguza msongo na kuleta utulivu. Lakini hakusafishi mapafu wala kutibu pumu, maambukizi au magonjwa sugu ya mapafu.

Njia muhimu zaidi ya kulinda mapafu ni kuepuka tumbaku na moshi wake, kupunguza kuathiriwa na vumbi na kemikali na kutafuta matibabu unapopata tatizo la kupumua. Mazoezi pia huboresha uwezo wa mwili kutumia oksijeni.

## Macho yanahitaji mapumziko kutoka kwenye skrini

Kutazama skrini muda mrefu kunaweza kusababisha macho kuchoka, kukauka na kuona kwa ukungu kwa muda. Pumzisha macho mara kwa mara kwa kutazama kitu kilicho mbali, pepesa macho na rekebisha mwanga wa skrini.

صفر

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Fikra nyingi katika jambo moja bila hatua hugeuka mzigo

**Kufikiri ni uwezo muhimu unaotusaidia kupanga, kuchambua matatizo na kufanya maamuzi. Lakini fikra zinapozunguka jambo lilelile bila kuzaa uamuzi, suluhisho au hatua, hugeuka mzigo. Hapo ndipo mtu huingia katika hali ya kufikiri kupita kiasi—overthinking—ambako akili inafanya kazi nyingi, lakini maisha hayasogei mbele.**

**Si kila tafakuri ndefu ni tatizo. Wanasayansi, waandishi na viongozi huhitaji muda wa kufikiri kwa kina. Tofauti ni kwamba tafakuri yenye manufaa hufikia hitimisho, swali jipya au hatua inayoweza kuchukuliwa. Kufikiri kupita kiasi hurudia hofu, makosa na uwezekano uleule bila kuleta mabadiliko.**

## Unalipa kodi kwa muda wako

Kufikiri kupita kiasi ni kama kodi inayokatwa moja kwa moja katika maisha. Dakika zinazotumika kurudia mazungumzo ya jana, kuhofia maoni ya watu au kutengeneza majanga ambayo hayajatokea haziwezi kurejeshwa.

Mtu anaweza kuonekana ametulia, lakini ndani ya akili yake kuna vikao visivyoisha: "Kwa nini alisema hivyo? Watanionaje? Nikikosea itakuwaje?" Tatizo si kuwa na mawazo hayo mara moja. Tatizo ni kuyapa mamlaka ya kutawala siku nzima.

## Usikimbie akili yako

Baadhi ya watu hujaribu kukimbia msongamano wa mawazo kwa kubadilisha mazingira, kusafiri, kulala kupita kiasi au kujizamisha katika mitandao ya kijamii. Njia hizo zinaweza kutoa nafuu ya muda, lakini haziwezi kuondoa chanzo. Popote unapokwenda, unaenda pamoja na akili yako.

Suluhisho si kuikimbia akili, bali kubadili uhusiano wako na mawazo. Jifunze kuyatazama kama matukio yanayopita, si amri zinazopaswa kutekelezwa wala ukweli unaopaswa kuaminiwa.

## Usichukulie kila wazo kuwa ukweli


Wazo linaweza kuwa hofu, kumbukumbu, dhana au tafsiri isiyo sahihi. Kwa hiyo, badala ya kusema, "Nitashindwa," jiulize: "Nina ushahidi gani?" Badala ya kudhani mtu amekudharau, tafuta maelezo mengine yanayowezekana.

Mawazo yanakuwa rahisi kuchunguzwa yanapotolewa kichwani. Yaandike, yazungumze na mtu unayemwamini au yageuze kuwa mchoro na mpango. Wazo likibaki kichwani linaweza kuonekana kubwa kuliko uhalisia wake.

## Badili maamuzi makubwa kuwa majaribio madogo

Watu wanaofikiri kupita kiasi mara nyingi hutaka uhakika kamili kabla ya kuchukua hatua. Lakini maisha hayatoi uhakika huo kila wakati. Badala ya kuendelea kujiuliza kama wazo litafanikiwa, lifanyie jaribio dogo.

Unataka kuanzisha biashara? Anza na wateja wachache. Unataka kuandika kitabu? Andika sura moja. Unataka kujifunza kozi mpya? Jaribu somo la mwanzo. Uhalisia unaweza kukupa jibu ambalo miezi ya kuwaza haiwezi kutoa.



## Tenga muda wa kuhangaika

Njia nyingine ni kutengeneza "kabati la wasiwasi." Tenga dakika 20 au 30 kila siku kwa ajili ya kuandika mambo yanayokusumbua. Jiulize lipi unaweza kulifanyia kazi, lipi linahitaji kusubiri na lipi haliko ndani ya uwezo wako.

Wasiwasi ukijitokeza nje ya muda huo, uandike na ujiahidi kuushughulikia wakati uliopangwa. Mbinu hii haiondoi mawazo kwa nguvu; inayawekea mipaka ili yasiteke siku nzima.

## Rekebisha yaliyopita, jenga yajayo

Kuna tofauti kati ya kutafakari yaliyopita na kuishi ndani yake. Ukiwaza kosa la zamani, jiulize kama unaweza kuomba msamaha, kurekebisha madhara au kujifunza somo. Kufanya hivyo kuna manufaa kuliko kujihukumu bila mwisho.

Vilevile, kuhofia yajayo hakujengi yajayo. Andika hatua moja unayoweza kuchukua leo. Kitendo kidogo kina nguvu zaidi kuliko mawazo makubwa yasiyo na utekelezaji.

## Jiondoe katikati ya kila jambo

Wakati mwingine kufikiri kupita kiasi huongezwa na dhana kwamba kila mtu anatuangalia, anatuzungumzia au anahukumu makosa yetu. Mara nyingi watu wengine nao wanashughulika na matatizo yao.

Hata hivyo, si sahihi kumwita kila anayefikiri kupita kiasi kuwa mwenye majivuno au ubinafsi. Sababu zinaweza kuwa hofu, uzoefu mgumu, kutaka ukamilifu au wasiwasi. Lakini kujifunza kutoyaweka maisha yote katikati ya nafsi yako kunaweza kuipunguzia akili mzigo.

Huwezi kuinyamazisha akili kwa kuipiga vita. Unaweza kuituliza kwa kuitazama, kuichunguza na kuielekeza katika hatua. Acha kupambana na kila wazo. Liulize linakufundisha nini—kisha amua kama linahitaji hatua, muda au kuachwa lipite.